JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI (DSEE) 2023

## KISWAHILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI (DSEE) 2023

# 721 KISWAHILI

*Kimechapishwa na:*

Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624, Dar es Salaam,
Tanzania.

**©Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

# YALIYOMO

DIBAJI .................... iv
1.0 UTANGULIZI .................... 1
2.0 TATHMINI YA KILA SWALI .................... 2
2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi .................... 2
2.1.1 Swali la 1: Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili .................... 2
2.1.2 Swali la 2: Zana za Kufundishia na Kujifunzia .................... 6
2.1.3 Swali la 3: Fasihi .................... 10
2.1.4 Swali la 4:Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili .................... 13
2.1.5 Maendeleo ya Kiswahili .................... 15
2.1.6 Swali la 6: Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili .................... 18
2.1.7 Swali la 7: Ufahamu. .................... 20
2.1.8 Swali la 8 Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Kiswahili .................... 23
2.1.9 Swali la 9: Uandishi .................... 26
2.1.10 Swali la 10: Upimaji .................... 30
2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha .................... 32
2.2.1 Swali la 11: Uhakiki wa Kazi za Fasihi .................... 33
2.2.2 Swali la 12: Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili .................... 38
3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU CHA WATAHINIWA KWA MADA .................... 43
4.0 HITIMISHO .................... 54
5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO .................... 54
KIAMBATISHO CHA PEKEE .................... 56

## DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa kuhitimu Stashahada ya Ualimu wa Sekondari kwa somo la Kiswahili mwaka 2023 imetayarishwa kwa lengo la kutoa mrejesho wa ufaulu wa watahiniwa kwa walimu tarajali, wakufunzi, watunga sera, wakuza mitaala, na wadau wengine wa elimu kuhusu namna watahiniwa walivyojibu maswali mbalimbali.

Taarifa hii inaonesha uchambuzi wa kila swali ambapo dosari mbalimbali zilizojitokeza wakati watahiniwa walipokuwa wanajibu maswali zimebainishwa. Dosari hizo zimeainishwa kwa kuonesha sampuli za majibu ya watahiniwa walioshindwa kujibu maswali kwa usahihi. Vilevile, ufafanuzi wa kina kuhusu jinsi watahiniwa walivyopata alama za juu, wastani na hafifu kwa kila swali na sampuli za majibu yao zimeoneshwa. Aidha, sababu mbalimbali ambazo zilichangia watahiniwa kuweza au kushindwa kujibu maswali kwa usahihi zimebainishwa.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa kuhitimu stashahada ya ualimu wa sekondari katika somo la Kiswahili mwaka 2023 unaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Watahiniwa hao walionesha uelewa wa kutosha kuhusu mada zilizotahiniwa na matakwa ya swali, matumizi sahihi ya lugha, na waliweza kutoa hoja sahihi zenye mifano dhahiri na kuzielezea katika mtiririko unaoleta mantiki. Pia, uchambuzi umeonesha kuwa, baadhi ya watahiniwa walipata alama za wastani kwa sababu walitoa majibu yasiyojitosheleza.

Hata hivyo, uchambuzi zaidi umeonesha kuwa watahiniwa wengine walikuwa na kiwango hafifu cha ufaulu kutokana na kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada zilizotahiniwa, dhana mbalimbali zinazohusiana na somo la Kiswahili na matakwa ya swali. Aidha, watahiniwa hao walikosa umahiri wa kujieleza katika mtiririko unaoleta mantiki na kushindwa kuandika kwa usahihi sehemu za utangulizi na hitimisho katika maswali ya insha.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa, taarifa hii itawawezesha walimu tarajali na wakufunzi kuelewa sababu za watahiniwa kujibu au kutokujibu vizuri maswali mbalimbali. Hivyo, kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji na utunzi wa mitihani mbalimbali kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukurani kwa wadau wote waliohusika katika kutayarisha taarifa hii.



Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la Kiswahili uliofanyika mwezi Mei, 2023 ulitungwa kwa kuzingatia Muhtasari wa Taaluma na Utaalamu wa kufundisha Kiswahili kwa Stashahada ya Ualimu ngazi ya Sekondari wa mwaka 2009. Mtihani huu ulikuwa na maswali 14 yaliyogawanyika katika sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali ya majibu mafupi na sehemu B ilikuwa na maswali ya insha. Maswali katika sehemu zote mbili yalitungwa kutoka katika mada za *Taaluma* na *Utaalamu wa Kufundisha Kiswahili*.

Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote kumi na nne (14) katika mtihani huu ambapo maswali kumi (10) yalitoka katika sehemu A na kila swali lilikuwa na uzito wa alama 4. Hivyo, jumla ya alama za sehemu hii ilikuwa 40. Katika sehemu B, mtahiniwa alipaswa kujibu maswali manne (4) ambapo kila swali lilikuwa na alama 15 na kufanya jumla ya alama katika sehemu hii kuwa 60.

Ufaulu wa watahiniwa umepangwa katika viwango vitatu; ambapo kiwango kizuri kilianzia alama 70 hadi 100, kiwango cha wastani alama 40 hadi 69 na kiwango hafifu alama 0 hadi 39. Aidha, chati za viwango vya ufaulu kiasilimia zimebainishwa kwenye kila swali ambapo ufaulu wa watahiniwa umebainishwa kwa kutumia rangi tatu. Rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano inawakilisha ufaulu wa wastani, na rangi nyekundu inawakilisha ufaulu hafifu.

Jumla ya watahiniwa 260 walisajiliwa kufanya mtihani wa Kiswahili kwa mwaka 2023. Kati yao, watahiniwa 258 ambao ni sawa na asilimia 99.2 walifanya mtihani na watahiniwa 2 sawa na asilimia 0.8 hawakufanya. Watahiniwa waliofaulu mtihani huu ni asilimia 99.6. Kwa upande mwingine, mtahiniwa 1 (0.4%) hakufaulu. Takwimu hizo zinadhihirisha kuwa, kiwango cha ufaulu wa watahiniwa kimeshuka ikilinganishwa na mwaka 2022 ambapo ufaulu wa watahiniwa ulikuwa asilimia 99.8.

## 2.0 TATHMINI YA KILA SWALI


Uchambuzi wa kila swali umefanyika ili kubaini jinsi ambavyo watahiniwa wameweza kujibu kwa usahihi au kushindwa maswali mbalimbali. Sababu za kina zilizowawezesha watahiniwa kujibu au kushindwa kujibu maswali hayo zimefafanuliwa. Aidha, vigezo vya uchambuzi wa maswali ya majibu mafupi na insha vimezingatiwa katika sehemu A na B kama ifuatavyo:

## 2.1 SEHEMU A: Maswali ya Majibu Mafupi

Swali litakuwa limejibiwa vizuri kama zaidi ya theluthi mbili (2/3) ya watahiniwa watakuwa wamepata alama kuanzia 3 hadi 4. Aidha, swali litakuwa limejibiwa vibaya iwapo theluthi mbili (2/3) ya watahiniwa watakuwa wamepata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Vilevile, swali litakuwa limejibiwa kwa kiwango cha wastani ikiwa idadi ya watahiniwa waliopata alama kuanzia 2 hadi 2.5 inazidi theluthi moja (1/3) na haikuzidi theluthi mbili (2/3).

### 2.1.1 Swali la 1: Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili


Swali hili lilimtaka mtahiniwa abainishe neno linalosababisha utata katika sentensi, kisha aoneshe maana mbili za sentensi hizo ambazo ni: (a) Bei ya paa ni shilingi elfu kumi na (b) Alimuandikia barua kaka yake. Watahiniwa 258 (100%) waliofanya mtihani walijibu swali hili ambapo asilimia 89.5 walipata alama 2 hadi 4. Hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kama inavyoonekana katika Chati Na. 1.




**Chati Na. 1:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1

Chati Na. 1 inaonesha kuwa watahiniwa 200 (77.5%) walipata alama 3 hadi 31 (12.0%) alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 27 (10.5%) walipata alama 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa asilimia 77.5 ya watahiniwa walipata ufaulu wa kiwango kizuri kutokana na uelewa wa kutosha waliokuwa nao wa mada ndogo ya *Utata katika Mawasiliano*. Hivyo, waliweza kutambua neno lililosababisha utata katika Sentensi mbili walizopewa na kubainisha maana mbili za sentensi hizo. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika neno 'paa' kuwa ndilo linalosababisha utata katika sentensi ya kipengele (a). Vilevile, alitoa maana mbili za sentensi hiyo kuwa ni: *(i) kifaa kinachotumika kuezeka nyumba* na *(ii) mnyama wa porini*. Katika sentensi ya kipengele (b), aliandika neno *alimuandikia* kuwa ndio neno linalosababisha utata na kutoa maana ya sentensi hiyo kuwa ni *(i) aliandika barua kwa niaba ya kaka yake* na, *(ii) aliandika barua ili aitume kwa kaka yake*. Kielelezo Na.1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


1

a Neno paa

i Paa ni mnyama afananae na mbuzi anaishi porini

ii Paa ni sehemu ya juu ya nyumba iliyo ezekwa kwa bati au makuti au majani

b Amemuandikia

i Kaka amesaidiwa kuandika barua na mtu mwingine badala ya kuandika yeye mwenyewe

ii Ujumbe wa barua umeandikwa kwenda kwa kaka ili ausome.


**Kielelezo Na.1.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 1.

Vilevile, watahiniwa wengine (12.0%) walipata alama za wastani. Miongoni mwao, wapo walioweza kubainisha neno linalosababisha utata katika sentensi zote mbili na kutoa maana mbili katika sentensi moja huku wakishindwa kufanya hivyo katika sentensi nyingine. Mathalani, mtahiniwa mmoja alijibu kwa kuandika kuwa *paa* ndilo neno linalosababisha utata katika sentensi ya kipengele (a) na maana zinazopatikana katika sentensi hiyo kuwa ni: *(i) kifaa cha kuezekea nyumba:* na *(ii) mnyama.* Hatahivyo, katika sentensi ya kipengele (b) aliweza kubainisha neno lililosababisha utata kuwa ni *"alimuandikia"* na kutoa maana mbili zisizo sahihi ambazo ni: *(i) alimuandikia kwa lengo la kumpenda:* na *(ii) Alimuandikia kaka yake barua*.

Aidha, watahiniwa wengine wa kundi hili wafanikiwa kubainisha neno linalosababisha utata katika sentensi zote mbili lakini walishindwa kueleza maana zinazopatikana katika sentensi hizo mbili. Pia, wengine waliweza kujibu kwa usahihi katika sentensi ya kipengele (b) ila wakashindwa kutoa maana za sentensi ya kipengele (*a)* kwa kuwa hawakuzingatia mantiki ya sentensi husika. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika maana ya sentensi hiyo kuwa ni: *(i) Enda hewani* na (ii) *kitendo cha kuondoa magamba kwenye samaki.* Kwa mantiki ya kawaida, kitendo cha *enda hewani* na *kuondoa magamba kwenye samaki* haviwezi kuuzwa bali kinachoweza kuuzwa ni paa kama kifaa cha kuezeka nyumba au paa kama mnyama kwa sababu watu huweza kununua kwa lengo la kuezeka nyumba au kutumia kama kitoweo mtawalia.

Hata hivyo, asilimia 10.5 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu kutokana na uelewa mdogo katika mada ndogo ya *Utata katika Mawasiliano*. Hivyo, walishindwa kubainisha maneno yaliyosababisha utata na kutoa maana mbili kwa kila sentensi katika sentensi mbili walizopewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo aliandika maana mbili sahihi za sentensi ya kipengele (a) kuwa ni: (i) *kwea angani*, na (ii) *Uzio uliopo juu ya nyumba* badala ya (i) *mnyama anayeishi porini*, na (ii) *kifaa kinachotumika kuezeka nyumba* ingawa alibainisha kwa usahihi neno lililosababisha utata katika sentensi hiyo kuwa ni *paa.* Mtahiniwa huyo alishindwa kuelewa kuwa mtu hawezi kukwea angani bali kwenye mti na kifaa kinachoezeka nyumba sio uzio bali uzio ni ua unaotengenezwa kuzunguka nyumba. Vilevile, mtahiniwa huyu alibainisha neno *barua* kuwa ndilo neno linalosababisha utata katika sentensi ya kipengele (b) badala ya *alimuandikia.* Aidha, alishindwa kutoa maana mbili za sentensi hiyo kwa kuandika: *(i) Barua kama waraka anaoandikiwa mtu kujua jambo fulani*, na *(ii) Barua ya kuomba kazi* badala ya *(i) aliandika barua kwa kaka yake*, na *(ii) Aliandika barua kwa niaba ya kaka yake* mtawalia. Kwa ujumla, mtahiniwa huyu aliweza kubainisha neno lililosababisha utata katika sentensi ya kwanza na kushindwa katika sentensi ya pili ingawa maana za sentensi zote mbili alizoandika hazikuwa sahihi. Hii inadhihirisha kuwa mtahiniwa huyu hakuwa na maarifa ya kutosha katika kubaini maneno mbalimbali yanayosababisha utata katika sentensi na maana zake.

Aidha, watahiniwa wengine waliweza kubainisha utata katika sentensi mojawapo na kutoa maana moja tu iliyosahihi, na kushindwa katika sentensi nyingine hivyo, kupata alama hafifu. Kielelezo Na.1.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha kwa usahihi neno lililosababisha utata na kutoa maana mbili za sentensi alizopewa.



1

(a) Neno lenye utata ni paa
- Paa ni kama mnyama
- paa ni kama elea angani


(b) Neno lenye utata ni kaka
- kaka ni jinsia ya kiume
- Kaka ni mtoto wa kiume

**Kielelezo Na.1.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 1.

Kielelezo Na.1.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha neno sahihi linalosababisha utata na maana mbili zinazopatikana katika sentensi ya kipengele (b). Aidha, aliweza kubainisha neno sahihi katika sentensi ya kipengele (a), kutoa maana sahihi moja, na kushindwa nyingine.

### 2.1.2 Swali la 2: Zana za Kufundishia na Kujifunzia


Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi hatua nne atakazozingatia iwapo atatumia redio kama mbinu ya kufundishia somo la Ufahamu wa Kusikiliza. Watahiniwa 258 (100%) walijibu swali hili ambapo asilimia 92.2 walipata alama za kiwango cha wastani hadi kizuri. Hivyo, swali hili lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati Na 2 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa.




**Chati Na. 2:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2

Chati Na. 2 inaonesha kuwa, watahiniwa 193 (74.8%) walipata alama 3 hadi 4, watahiniwa 45 (17.4%) alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 20 (7.8%) walipata alama 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa asilimia 74.8 ya watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Watahiniwa hawa walielezea kwa usahihi hatua 3 hadi 4 za kuzingatia iwapo watatumia redio kama mbinu ya kufundishia somo la ufahamu wa kusikiliza. Watahiniwa hao, walitoa majibu kama vile, *kuwaandaa wanafunzi katika mazingira tulivu ili waweze kusikiliza kwa makini*, *kufafanua mambo mbalimbali yanayowatatiza wanafunzi wakati wa kipindi*, *kuhakikisha na kusimamia wanafunzi wanatekeleza maelekezo (au amri) kutoka kwa msemaji wa redioni*, na *kuwaongoza wanafunzi kufanya marejeo kuhusu maudhui yaliyowasilishwa kwa kuuliza maswali yatakayotokana na habari waliyosikiliza*. Kielelezo Na. 2.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



| | |
|---|---|
| 2 | (i) Kuwaongoza wanafunzi wawe na utulivu. |
| | (ii) kuwahimiza wanafunzi waweze kusikiliza |
| | kwa makini redio inachozungumza |
| | (iii) kuwaongoza wanafunzi kufuatilia |
| | kwa makini kipengele kimoja baada |
| | ya kingine kinachozungumzwa kwenye |
| | redio |
| | (iv) kuwauliza wanafunzi nini wamesikiliza |
| | kutoka kwenye redio. |

**Kielelezo Na.2.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 2.


Vilevile, watahiniwa wengine (17.4%) walipata alama za wastani kutokana na maarifa ya wastani waliyokuwa nayo kuhusiana na mada ndogo ya *Mbinu Anuai za Kufundishia Somo la Kiswahili*. Hivyo, walibainisha hatua mbili sahihi kati ya nne zilizohitajika na nyingine mbili zisizo sahihi. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walichanganya hatua za kuzingatia iwapo mwalimu atatumia redio kama mbinu ya kufundisha ufahamu wa kusikiliza na mambo ya kuzingatia iwapo watatumia redio kama zana ya kufundishia mada hiyo. Mtahiniwa mmoja aliandika hoja mbili sahihi ambazo ni: *nitatambulisha mada kwa wanafunzi* na *nitawaelekeza wanafunzi kusikiliza kwa makini*; na hoja mbili zisizo sahihi ambazo ni*; Kuhakikisha redio inasikika vizuri na kurekodi hadithi redioni*. Hivyo, mtahiniwa huyo kupata alama za wastani.

Aidha, watahiniwa wengine walichanganya hatua za kuzingatia iwapo watatumia redio kama mbinu ya kufundishia ufahamu wa kusikiliza na mambo ya kuzingatia wakati wa kuchagua hadithi ya kufundishia ufahamu wa kusikiliza kama vile *inatakiwa iendane na tamaduni na umri wa wanafunzi* na *iwe na lugha inayoendana na ngazi ya wanafunzi*. Hii inadhihirisha kuwa watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa wastani kuhusiana na mbinu anuwai za kufundisha somo la ufahamu wa kusikiliza.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (7.8%) walipata alama hafifu katika swali hili. Wengi wao walionesha kuwa na uelewa mdogo juu ya hatua za kuzingatia iwapo mwalimu atatumia redio kama mbinu

ya kufundisha ufahamu wa kusikiliza jambo lililowasababisha kujibu kinyume cha matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hatua za ufundishaji wa somo la ufahamu wa kusikiliza ambazo ni *utangulizi, maarifa mapya, kukazia maarifa, tafakuri na hitimisho* badala ya hatua atakazozingatia mwalimu iwapo atatumia mbinu ya redio kufundishia somo la ufahamu wa kusikiliza kama vile *kuwaandaa wanafunzi katika mazingira tulivu ili waweze kusikiliza kwa makini*, *kufafanua mambo mbalimbali yanayowatatiza wanafunzi wakati wa kipindi*, *kuhakikisha na kusimamia wanafunzi wanatekeleza maelekezo (au amri) kutoka kwa msemaji wa redioni*, na *kuwaongoza wanafunzi kufanya marejeo kuhusu maudhui yaliyowasilishwa kwa kuuliza maswali yatakayotokana na habari waliyosikiliza*.

Aidha, watahiniwa wengine walieleza mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa redio kama zana ya kufundishia somo la ufahamu wa kusikiliza ambayo ni *kuhakikisha kuwa redio haina changamoto, kuhakikisha sauti ya redio inasikika kwa wanafunzi wote*, *kuzingatia wanafunzi wenye mahitaji maalumu,* na *kutafuta namna ya upatikanaji wa redio.* Kielelezo Na. 2.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa mmojawapo wa kundi hili.



2
(i) Kutunza kumbukumbu
Wakati wa kutumia redio katika ufundishaji Mwanafunzi huweza kutunza kumbukumbu ya kudumu.
(ii) Huweza kutafakari
Katika Mbinu hii ya kufundishia redio Mwanafunzi huweza kutafakari kwa kina kile anachokisikia.
(iii) Tathimini
Pia huweza kufanya tathmini kuwa ni wangapi wameweza kuelewa somo vizuri kwa kutumia Mbinu hii.
(iv) Maarifa: Katika mbinu hii ya kufundisha kwa kutumia redio Mwanafunzi huwa na Maarifa aliyoyapata kwa kupitia redio.

**Kielelezo Na.2.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 2.

Katika kielelezo Na. 2.2, mtahiniwa aliandika faida atakazozipata mwanafunzi iwapo mwalimu atafundisha kwa kutumia mbinu ya redio badala ya hatua atakazozingatia ikiwa atafundisha somo la ufahamu wa kusikiliza kwa kutumia mbinu hiyo.

### 2.1.3 Swali la 3: Fasihi

Swali lilimtaka mtahiniwa kutumia hoja nne kufafanua sababu zinazoifanya fasihi kuchukuliwa kama kioo cha jamii. Watahiniwa 258 (100%) waliofanya mtihani walijibu swali hili. Kati yao, asilimia 70.9 walipata ufaulu wa kiwango cha wastani hadi kizuri na kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati Na. 3 inaonesha ufaulu wa watahiniwa.





**Chati Na. 3:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3

Chati Na. 3 inaonesha kuwa, watahiniwa 98 (38.0%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5, 85 (32.9%) alama 3 hadi 4 na watahiniwa 75 (29.1%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, baadhi ya watahiniwa (38.0%) walipata alama za wastani katika swali hili. Watahiniwa hao, walikuwa na uelewa wa wastani kuhusiana na mada ya *Fasihi*. Hivyo, walishindwa kutoa majibu yanayojitosheleza katika kueleza sababu zinazoifanya fasihi kuchukuliwa kama kioo cha jamii. Miongoni mwao, waliandika hoja mbili sahihi na mbili zisizo sahihi ambapo waliandika dhima za fasihi kwa ujumla badala ya kuonesha namna ambavyo dhima hizo zinaakisi uhalisia wa jamii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja sahihi ambazo ni *fasihi ina kazi ya kuiokosoa jamii* na

*kuielimisha* na hoja mbili zisizo sahihi ambazo ni *fasihi inarithisha na kuhifadhi amali za jamii* na *hutumika kama chanzo cha mapato kwa watunzi wa kazi mbalimbali*. Watahiniwa wengine wa kundi hili waliweza kueleza hoja mbili sahihi kati ya nne na wengine walichanganya sababu zinazoifanya fasihi kuwa kioo cha jamii na sifa za fasihi simulizi. Kwa ujumla, watahiniwa hawa walishindwa kutambua kuwa siyo dhima zote za fasihi zinafafanua fasihi kama kioo cha jamii.


Aidha, asilimia 32.9 ya watahiniwa walijibu swali hili vizuri kwa kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Fasihi* na matakwa ya swali. Hivyo, waliweza kueleza sababu 3 au 4 zinazoifanya fasihi kuchukuliwa kama kioo cha jamii. Miongoni mwa majibu yao ni kama vile *fasihi ina kazi ya kuikosoa jamii pale inapokwenda kinyume na matakwa ya jamii*, *kuielimisha jamii yale ambayo hawayafahamu*, *kuiongoza jamii pale inapokwenda kinyume na taratibu zilizokubaliwa*, *kuonesha aina zote za udhalimu*, na *kutabiri mambo mabaya yanayoweza yakajitokeza katika jamii*. Kielelezo Na. 3.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kueleza sababu nne zinazoifanya fasihi kuwa kioo cha jamii.


3 i) Kuyadili mambo yaliyoko katika jamii, mfano suala la ulevi umaskini.
ii) Kuasa jamii kuachana na utamaduni au mambo ambao yamepitwa na wakati. Ili yasiendelee kunyanyasa watu. Mfano suala la kupata elimu na la watoto wa kiume tu, wakati hata wa kike nao wanahitaji sawa.
iii) Kutoa elimu katika jamii, mfano ili kuendelea kiuchumi serikali au jamii haina budi kupinga unyonyaji.
iv) Kuadabisha jamii kwa mambo inayofanya ambayo yako kinyume na utu wa binadamu. Mfano ukeketaji wa wanawake, fasihi hutoa adhabu iwapo wataendelea kufanya hivyo watachukuliwa hatua kali za kisheria.

**Kielelezo Na. 3.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 3.

Uchambuzi zaidi wa takwimu unaonesha kuwa asilimia 29.1 ya watahiniwa walikosa uelewa wa kutosha kuhusu mada ya *Fasihi*. Hivyo,

walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5. Watahiniwa hao, walishindwa kueleza sababu 4 zinazoifanya fasihi kuchukuliwa kama kioo cha jamii. Kwa hiyo, walieleza hoja dhaifu ambazo hazithibitishi kuwa fasihi ni kioo cha jamii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa *fasihi ni kioo cha jamii kwa sababu watunzi ni wanajamii, yanayoongelewa katika fasihi yapo kwenye jamii, kazi ya fasihi inaandikwa kwa wanajamii* na *inamilikiwa na wanajamii*. Mtahiniwa huyu aliandika hoja hizo kwa sababu alielewa kuwa swali lilimtaka kuonesha uhusiano uliopo kati ya fasihi na jamii badala ya kueleza sababu nne zinazoifanya fasihi kuchukuliwa kama kioo cha jamii. Aidha, watahiniwa wengine walibainisha sifa za fasihi simulizi. Mathalani, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa sababu za fasihi kuwa kioo cha jamii ni *hutumia lugha bunifu katika kuwasilisha kazi ya kisanaa*, *hufanyika sehemu ya matukio kufanyika*, *hutumia wahusika wanyama na binadamu*, *na hadhira* na *fanani huonana ana kwa ana*. Aidha, watahiniwa wengine waliweza kueleza sababu moja tu kati ya nne zilizohitajika huku wengine wakitoa sababu 2 bila kueleza. Hivyo, kusababisha watahiniwa hawa kupata alama hafifu. Kielelezo Na.3.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa mmojawapo.


3

(i) Huelimisha jamii

(ii) Hukosoa jamii

(iii) Huburudisha jamii.

(iv) Hutunza amali za jamii

**Kielelezo Na. 3.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 3.

Kielelezo Na. 3.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeandika dhima za fasihi katika hoja ya (iii) na (iv) badala ya kueleza sababu zinazoifanya fasihi kuchukuliwa kama kioo cha jamii. Aidha, aliweza kuandika sababu sahihi katika hoja ya (i) na (ii) ingawa hakueleza hoja zinazothibitisha fasihi kuchukuliwa kama kioo cha jamii.

### 2.1.4 Swali la 4: Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili


Swali lilimtaka mtahiniwa kuelezea namna kitabu cha ziada cha somo la Kiswahili kitakavyomsaidia kufundisha somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa kidato cha pili. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 258 (100%) ambapo watahiniwa 256 (99.2%) walijibu vizuri na kupata alama 2 hadi 4. Hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na.1.

**Jedwali Na. 1:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 4

| Na | Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|---|
| 1. | 3 - 4 | 255 | 98.8 |
| 2. | 2 – 2.5 | 1 | 0.4 |
| 3. | 0-1.5 | 2 | 0.8 |

Jedwali Na. 1 linaonesha kuwa, watahiniwa 255 (98.8%) walipata alama 3 hadi 4, 2 (0.8%) alama 2 hadi 1.5 na mtahiniwa 1 (0.4%) alipata alama 2

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, watahiniwa wengi (98.8%) walipata kiwango kizuri cha ufaulu katika swali hili. Waliweza kuelezea jinsi kitabu cha ziada kitakavyoweza kuwasaidia kufundisha somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa kidato cha pili. Hivyo, waliandika hoja 3 hadi 4 kwa usahihi. Miongoni mwa majibu sahihi ya watahiniwa ni kama vile *kitamsaidia kupata maarifa mapana zaidi nje ya yale yaliyopo kwenye kitabu cha kiada, kusaidia kupata mazoezi na maswali mbalimbali ya kupimia uelewa wa wanafunzi, kupata maudhui ya ziada ambayo hayakufafanuliwa kwenye kitabu cha kiada*, na *kutumika kama kitabu cha rejea wakati wa kuandika azimio la kazi na andalio la somo la mwalimu*. Hii inathibitisha kuwa watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili* kama inavyothibitishwa katika kielelezo Na. 4.1.


4

i) Kitabu cha ziada humsaidia Mwalimu katika kupata mazoezi mbali mbali

ii) Kitabu cha ziada humsaidia Mwalimu katika kupata Maarifa mpya yanayoenda na na yale yaliyoko kwenye kitabu cha kiada.

iii) Humsaidia Mwalimu katika kupata picha, michoro pamoja na vielelezo mbalimbali hasa yale yanayoendana na mada inayofundishwa darasani

iv) Humsaidia Mwalimu kuwaandaa wanafunzi wake kuwapa mazoezi yakutosha na hatimaye kufaulu Mtihani wa Mwisho.


**Kielelezo Na. 4.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 4.

Pamoja na watahiniwa wengi kufanya vizuri katika swali hili, watahiniwa 2 (0.8%) walipata alama hafifu kutokana na kukosa uelewa wa kutosha juu ya mada ya *Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili*. Hivyo, walishindwa kueleza namna ambavyo kitabu cha ziada kitawasaidia kufundisha somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa kidato cha pili. Mtahiniwa mmoja alichanganya jinsi kitabu cha ziada kitakavyoweza kumsaidia kufundisha na kazi za kamusi. Hivyo, aliandika hoja moja sahihi ambayo ni *kitamsaidia kuandaa nukuu za somo la Kiswahili* na hoja tatu zisizo sahihi ambazo ni k*uangalia maana mbalimbali za misamiati, asili ya maneno na kategoria ya maneno*. Aidha, mtahiniwa mwingine aliandika hoja mbili sahihi kati ya nne bila kuelezea.

Kwa upande mwingine, mtahiniwa mmoja tu (0.4%) ndiye aliyepata alama za wastani katika swali hili kwani alibainisha hoja mbili tu kwa usahihi kati ya nne. Hoja zilizoandikwa na mtahiniwa huyo ni *kuongeza maarifa ya ziada kwa mwalimu na huweza kutumiwa kama zana mfano kuonesha kipengele cha fani katika mada ya fasihi*.

### 2.1.5 Swali la 5: Maendeleo ya Kiswahili

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutumia hoja mbili za Kisayansi kukubaliana na kauli inayosema kuwa *Asili ya lugha ya Kiswahili ni Kibantu* kisha kutoa mfano kwa kila hoja. Watahiniwa 258 (100%) walijibu swali hili. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni kizuri kwani asilimia 82.9 walipata alama 2 hadi 4. Hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kama inavyothibitishwa katika Chati Na 4.





**Chati Na. 4:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5

Chati Na. 4 inaonesha kuwa, watahiniwa 190 (73.6%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4, watahiniwa 44 (17.1%) alama kuanzia 0 hadi 1.5 na 24 (9.3%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, watahiniwa wengi (73.6%) walijibu vizuri swali hili. Hii imetokana na kuwa na uelewa wa kutosha juu ya ushahidi wa kisayansi unavyothibitisha kuwa asili ya lugha ya Kiswahili ni Kibantu. Watahiniwa hao, waliweza kutoa hoja mbili sahihi na mfano mmoja katika kila hoja. Miongoni mwa majibu ya watahiniwa katika kundi hili ni kama vile *kufanana kwa msamiati baina ya lugha ya Kiswahili na zile za Kibantu*. Kwa mfano, Kiswahili- *mtu*; Kiyao – *mundu*; na Kihehe - *munu*, *kufanana kwa maumbo ya maneno yaliyopo kati ya lugha ya Kiswahili na zile za Kibantu*. kwa mfano, *Kiswahili - a-na-chez-a*; *Kipare - a- vin-a*; na *Kihehe -i- kin-a*, na *Kufanana kwa miundo ya tungo kati ya zile za lugha ya Kiswahili na zile za lugha nyingine za Kibantu*. Kwa mfano:

*Kiswahili: Mtoto anaimba vizuri.*
*N T E*
*Kihehe: Umwana akwimba lunofu.*
*N T E*
*Kiyao: Mwanache akwimba ucheneche.*
*N T E*

Kielelezo Na. 5.1 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyejibu vizuri swali hili na kupata alama za juu.


5 (i) Msamiati; kwa kiasi kikubwa msamiati wa lugha ya kiswahili na lugha za kibantu unafanana. Hiki ikizingatiwa kuwa kibantu kinachangia asilimia 64 za msamiati wa lugha ya kiswahili. Hivi ndivyo msamiati wa luga ya kiswahili unafanana.

| Kiswahili | Kiha |
|---|---|
| Mama | Mawe. |
| Mwana | umwana. |

(ii) Ngeli za nomino; nomino za kiswahili zina mambo ya umoja na wingi kama zilivyo nomino za lugha za kibantu kwa mfano;


| Kiswahili (umoja) | Kiswahili wingi |
|---|---|
| Mwana | watoto |
| kiha umoja | kiha wingi |
| umwana | abhana |

**Kielelezo Na. 5.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 5.

Hata hivyo, asilimia 17.1 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata kiwango hafifu cha ufaulu kutokana na uelewa wao mdogo kuhusu ushahidi wa kisayansi unaothibitisha kuwa asili ya Kiswahili ni Kibantu. Hivyo, walielezea nadharia nyingine za asili ya lugha ya Kiswahili badala ya hoja nne za kisayansi zinazothibitisha kuwa asili ya Kiswahili ni Kibantu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *Kiswahili asili yake ni Kongo; lugha ya Kiswahili imetokana na wakongo waliosambaa upwa wa pwani ya Afika Mashariki*, na *asili ya lugha ya Kiswahili ni Kiarabu kwa sababu Kiswahili kina msamiati mwingi wa Kiarabu* badala ya *kufanana kwa msamiati baina ya lugha ya Kiswahili na zile za Kibantu*.

Aidha, mtahiniwa mwingine alielezea kuwa: *Asili ya Kiswahili ni pijini kwa sababu Waarabu na watu wa Pwani ya Afrika Mashariki walitumia lugha ambayo siyo Kiswahili wala Kiarabu. Lugha hiyo inasemekana ni Kiswahili* na *Kiswahili ni lugha ya vizalia kwa sababu iliongelewa na uzao uliotokana na Waarabu na watu wa Pwani ya Afrika Mashariki*.

Kwa ujumla, watahiniwa hawa hawakuelewa kuwa ushahidi wa kisayansi unathibitisha kuwa asili ya lugha ya Kiswahili ni kibantu katika nadharia ya “Kiswahili ni Kibantu.” Kwa hakika majibu hayo yanafafanua nadharia nyingine zinazoelezea asili ya lugha ya Kiswahili badala ya kutumia hoja za kisayansi kufafanua kuwa asili ya lugha ya Kiswahili ni kibantu. Pia, kuna watahiniwa wengine waliweza kuandika hoja mbili sahihi ila wakashindwa kutoa ufafanuzi wowote kuhusiana na hoja hizo na mifano kama yalivyokuwa matakwa ya swali. Hivyo, watahiniwa hao walipata alama hafifu. Mathalani, mtahiniwa mmoja alibainisha hoja ya *Kuwapo kwa misamiati inayoyotokana na lugha za Kibantu na tungo za sentensi za Kiswahili* bila kutoa ufafanuzi zaidi. Kielelezo Na 5.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa mmojawapo aliyejibu kinyume cha matakwa ya swali.



i) Ushahidi wa AL-IDRIS, huyu ni mtu amb
aye anaamini kuwa kiswahili ni kibantu kwa
sababu neno "Zanzibar" limetokana na Ubantu
wa kiswahili na kuitwa "Zenji"


ii) Ushahidi wa MARCO-polo, huu ni ushahidi
wa kisayansi ambao marco polo anaamini kuwa
asili ya lugha ya kiswahili ni pwani ya Afrika
Mashariki ndiko kiswahili kilipoanzia.

**Kielelezo Na. 5.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 5.

Katika kielelezo Na. 5.2, mtahiniwa alielezea hoja za kihistoria kuthibitisha kuwa asili ya Kiswahili ni Kibantu badala ya kuelezea hoja za kisayansi kama yalivyokuwa matakwa ya swali.

### 2.1.6 Swali la 6: Zana za Kufundishia na Kujifunzia Somo la Kiswahili

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufafanua mambo manne ya kuzingatia wakati wa kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia. Watahiniwa 258 (100%) walijibu swali hili. Miongoni mwao, watahiniwa 253 (98.1%) walipata alama 2 hadi 4. Hivyo, swali hili lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati Na. 5 inafafanua zaidi viwango vya ufaulu wa watahiniwa.




**Chati Na. 5:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6

Chati Na. 5 inaonesha kuwa watahiniwa 219 (84.9%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4, watahiniwa 34 (13.2%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5 na 5 (1.9%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, asilimia 84.9% ya watahiniwa walijibu vizuri swali hili. Waliweza kufafanua mambo sahihi 3 hadi 4 yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia. Majibu ya watahiniwa hao ni kama vile *zana lazima iendane na umri wa walegwa, iendane na mada ya somo husika, izingatie ukubwa wa darasa, ionekane vizuri na kuvutia,* na *iendane na mada husika na muhtasari wa somo*. Kielelezo Na.6.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

| 6 | |
|---|---|
| (i) | Kuzingatia mada na malengo mahususi ya mada |
| | husika lazima yaendane na zana inayoandaliwa. |
| (ii) | Zana inatakiwa iandaliwe kwa kuzingatia ukubwa |
| | wa darasa na wingi wa wanafunzi ili iweze kukidhi |
| | kile kilichokusudiwa |
| (iii) | Kuzingatia ukubwa unaoweza kuonekana vizuri kwa |
| | wanafunzi wote |
| (iv) | Lazima zana iendane na umri na hali za wanafu |
| | nzi yaani wenye mahitaji maalumu kama vile |
| | uoni hafifu, wasioona na usikivu hafifu. |


**Kielelezo Na. 6.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 6.

Vilevile, asilimia 13.2 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kwani walikuwa na uelewa wa wastani kuhusiana na mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia. Miongoni mwao, wapo waliobainisha hoja mbili sahihi na nyingine zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa zana za ufundishaji na ujifunzaji na umuhimu wa kutumia zana. Wengine waliandika hoja nne sahihi lakini hawakuweza kuelezea. Hivyo, walipata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, asilimia 1.9 ya watahiniwa walipata alama 0 hadi 1.5 kwa kuwa walikuwa na uelewa mdogo juu ya mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili. Hivyo, watahiniwa hawa walishindwa kubainisha mambo ya kuzingatia wakati wa kutengeneza zana. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika mambo anayopaswa kufanya mwalimu kabla ya kutumia zana darasani kama vile *matayarisho ya zana, kujua itatumika katika hatua gani, kujaribu kuitumia akiwa peke yake*, na *kutathmini wingi wa wanafunzi wake kabla ya kutumia* badala ya mambo manne ya kuzingatia wakati wa kuandaa zana ambayo ni *zana lazima iendane na umri wa walegwa, iendane na mada ya somo husika, izingatie ukubwa wa darasa, ionekane vizuri na kuvutia, mada husika na muhtasari wa somo*.

Vilevile, watahiniwa wengine walijibu kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika aina za zana za kufundishia na kujifunzia badala ya mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia. Aidha, watahiniwa wengine waliandika hoja

moja sahihi na nyingine zisizo sahihi na wengine waliandika hoja sahihi mbili bila kufafanua kwa ufupi. Hivyo watahiniwa hawa walipata alama hafifu. Kielelezo Na.6.2 .ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia.


6

i) Muhtasari, hili ni jambo muhimu sana wakati wa kuanda zana ya kufundishia na kujifunzia kwa sababu huu ni muongozo wa ufundishaji na ujifunzaji.

ii) Kitabu cha kiada, hiki ni kitabu anachotumia mwalimu kufundishia. Hivyo basi, wakati wa kuandaa zana hiki kitabu ni muhimu sana.

iii) Azimio la kazi, mwalimu anapoandaa zana lazima awe na Azimio la kazi ili _ _ anachoandaa kama zana lendane na Azimio la kazi


iv) Andalio la somo, mwalimu anapoandaa zana lazima awe na Andalio la somo

**Kielelezo Na. 6.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 6.

Katika kielelezo Na. 6.2, mtahiniwa alishindwa kubainisha mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia badala yake akabainisha vifaa vya mtaala anavyopaswa kuvitumia mwalimu wakati wa kuandaa somo la Kiswahili.

### 2.1.7 Swali la 7: Ufahamu

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kutumia hoja nne kufafanua kwa ufupi umuhimu wa kufundisha somo la ufahamu wa kusoma kwa wanafunzi wa kidato cha I- IV. Watahiniwa 258 (100%) walifanya swali hili. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa kilikuwa hafifu kwani watahiniwa 83 (32.2%) ndio waliopata alama 2 hadi 4. Chati Na 7 inafafanua zaidi viwango vya ufaulu vya watahiniwa.





**Chati Na. 6:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7

Chati Na. 6 inaonesha kuwa, watahiniwa 175 (67.8%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5, watahiniwa 63 (24.4%) alama kuanzia 2 hadi 2.5 na watahiniwa 20 (7.8%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4.

Asilimia 67.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili, walipata alama hafifu. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa mdogo kuhusu umuhimu wa kufundisha somo la ufahamu wa kusoma kwa wanafunzi wa kidato cha I – IV. Wengi wao waliandika stadi nne za lugha badala ya umuhimu wa kufundisha somo la ufahamu wa Kusoma. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *kuzungumza, kusikiliza, kuandika*, na *kusoma* badala ya *husaidia kutambua maandishi na maana iliyomo, hukuza kasi na wepesi katika kusoma, hujenga moyo wa kupenda kusoma, huimarisha uwezo kugundua, kuchagua na kupanga mawazo muhimu yaliyopo katika habari iliyosomwa na huimarisha kiwango cha matumizi yake ya lugha*. Mtahiniwa huyo aliandika majibu hayo kwa sababu somo la ufahamu linahusisha shughuli mbalimbali zinazowezesha kukuza stadi hizo za lugha.

Aidha, watahiniwa wengine walielezea umuhimu wa elimu badala ya umuhimu wa kufundisha somo la ufahamu wa kusoma. Mathalani, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa: *ufahamu husaidia kupata maarifa mbalimbali, kujua historia ya jamii fulani, kujikomboa kutoka katika uchumi mdogo*, na *kujiamini katika jamii*. Hii inadhihirisha kuwa

mtahiniwa huyo alihusianisha ufahamu wa kusoma na mchakato wa kujifunza ambapo mtu husoma vitabu mbalimbali kwa lengo la kupata maarifa ya jambo fulani kwa sababu ufahamu wa kusoma huhusisha kitendo cha kusoma kisha kujibu maswali kutokana na habari iliyosomwa. Vilevile, watahiniwa wengine walielezea umuhimu wa kufundisha somo la fonolojia kwa wanafunzi kwa sababu fonolojia inahusika na matamshi ya maneno na mwanafunzi anaposoma hutamka maneno . Pia, watahiniwa wengine walifafanua hoja moja kwa usahihi kati ya nne zilizohitajika hivyo, kupelekea kupata alama hafifu. Kielelezo Na 7.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kufafanua kwa usahihi sababu nne za kufundisha ufahamu wa kusoma.


7

i) Kwa sababu husaidia kukuza stadi ya kuandika darasani mfano kuandika insha na kuelewa jinsi inavyosomwa

ii) Husaidia kujua stadi ya kuzingatia alama mbalimbali katika maandishi ya ufahamu

iii) Ufahamu wa kusoma husaidia kumjengea mwanafu na maarifa mapya

iv) Husaidia kumuwekea mwanafunzi kumbukumbu za kusoma darasani


**Kielelezo Na. 7.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 7.

Kielelezo Na. 7.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeeleza umuhimu wa kusoma matini mbalimbali kwa mwanafunzi katika hoja ya (ii), (iii) na (iv) badala ya umuhimu wa kufundisha somo la ufahamu kwa wanafunzi wa kidato cha I – IV. Aidha, alielezea umuhimu wa kufundisha somo la uandishi katika hoja ya (i).

Pamoja na hayo, asilimia 24.4 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani kutokana na uelewa wa wastani waliokuwa nao kuhusiana na mada ndogo ya *Ufahamu wa Kusoma*. Hivyo, walifafanua kwa ufupi umuhimu wa kufundisha ufahamu wa kusoma kwa hoja mbili tu na kushindwa nyingine na wengine waliishia kufafanua hoja mbili sahihi huku wakichanganya na umuhimu wa kusoma matini mbalimbali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alifafanua hoja mbili sahihi ambazo ni *husaidia kukuza stadi za kusoma,* na

*husaidia kukuza stadi ya utulivu na usikivu*. Aidha, mtahiniwa huyo alieleza hoja zisizo sahihi ambazo ni *kuelewa kwa urahisi kile wanachokisoma* na *kusaidia kupata maarifa mahsusi*.


Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (7.8%) walijibu swali hili vizuri. Watahiniwa hao, waliweza kufafanua kwa ufupi umuhimu wa kufundisha somo la ufahamu wa kusoma kwa wanafunzi wa kidato cha I –IV kwa hoja nne. Miongoni mwa majibu sahihi yaliyotolewa na watahiniwa hao ni pamoja na *kusaidia kutambua maandishi na maana iliyomo, kukuza kasi na wepesi katika kusoma, Hujenga moyo wa kupenda kusoma, huimarisha uwezo wa kugundua, Kuchagua na kupanga mawazo muhimu yaliyopo katika habari iliyosomwa* na *Huimarisha kiwango cha matumizi yake ya lugha*. Kielelezo Na. 7.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


7
(i) Ufahamu wa kusoma huwasaidia wanafunzi kupata maarifa yaliyo wasilishwa kwa njia ya maandishi. Mfano kupitia ufahamu wa kusoma kitabu mwanafunzi hupata maarifa yaliyomo kwenye kitabu hicho.
(ii) Huwajengea wanafunzi tabia ya kupenda kujisomea vitabu mbalimbali hivyo kuongeza maarifa mengi.
(iii) Huwawezesha wanafunzi kujua namna ya kusoma kwa kuzingatia kanuni za uandishi mfano nukta, alama ya kuuliza na matumizi ya nukta, ambavyo hupatikana katika ufahamu wa kusoma.
(iv) Huwasaidia wanafunzi kufahamu namna ya kubaini mawazo makuu katika habari wanayoisoma.

**Kielelezo Na. 7.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 7.

### 2.1.8 Swali la 8: Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Kiswahili


Mtahiniwa alitakiwa kuchambua kwa ufupi mambo manne yanayoweza kufanywa na mwalimu katika hatua ya utangulizi wa somo anapofundisha mada ndogo ya *Aina za Maneno* (Nomino). Watahiniwa 258 (100%) walijibu swali hili ambapo asilimia 73.3 walipata alama 2 hadi 4. Hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yenye kiwango kizuri cha ufaulu kama inavyoonekana katika Chati Na. 7.




**Chati Na. 7:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8

Chati Na. 7 inaonesha kuwa, watahiniwa 148 (57.4%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4, watahiniwa 69 (26.7%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5 na 41 (15.9%) alama kuanzia 2 hadi 2.5.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa zaidi ya nusu ya watahiniwa (57.4%) walijibu vizuri swali hili kwa kuwa walielewa mada ndogo ya *Andalio la Somo*. Hivyo, waliweza kuelezea kwa ufupi mambo manne yanayoweza kufanywa na mwalimu katika hatua ya utangulizi wanapofundisha mada ndogo ya *Aina za Maneno* (nomino). Watahiniwa hawa walitoa majibu kama vile *kujenga utayari wa wanafunzi*, *kuwapa wanafunzi chemsha bongo/bungua bongo kuwauliza maswali mafupimafupi yanayohusu nomino*, *kuuliza maswali ya mada iliyopita*, na *kuuliza maswali mepesi yanayochokonoa somo jipya*. Kielelezo Na. 8.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa mmojawapo wa kundi hili.



8 (i) Kutambulisha mada kwa kuwauliza ma
swali. mfano kuwauliza wana funzi wawi
li majina na kuyaandika ubaoni.
(ii) Kuwaimbisha wimbo unaotaja aina za
maneno. mfano. wimbo wa nomino wa matunda,
Parachichi, Papai, tikitiki maji, maembe na
mapera x2
(iii) Kuwauliza maswali kuhusu somo lililo
tangulia.
(iv) Kusimu-lia kahistoria kafupi kanakohusu
aina za maneno na baadaye kuuliza
maswali ili waweze kubaini ulichokuwa
umekilenga. kwa kufanya ubashiri.

**Kielelezo Na. 8.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 8.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata alama kuanzia 0 hadi 1.5 walikuwa asilimia 26.7. Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mada ndogo ya *Andalio la Somo* kwa sababu walishindwa kuchambua mambo manne anayoweza kuyafanya mwalimu katika hatua ya utangulizi wakati anapofundisha *Aina za Maneno* (Nomino). Miongoni mwao, wapo walibainisha mambo anayopaswa kufanya mwalimu katika hatua zote za somo badala ya mambo anayopaswa kufanya katika hatua ya utangulizi pekee. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *katika hatua ya utangulizi nitauliza maswali ya mada iliyopita, hatua ya maarifa mapya: nitatumia zana ya kadi za maneno kuwaongoza wanafunzi kubainisha aina za nomino, maana na mifano*, na *katika hatua ya tafakuri nitawaongoza wanafunzi kutaja nomino mbalimbali zinazopatikana katika mazingira yao ya kila siku na kusema ni ya aina gani* badala ya *kujenga utayari wa wanafunzi*, *kuwapa wanafunzi chemsha bongo/bungua bongo kuwauliza maswali mafupimafupi yanayohusu nomino*, *kuuliza maswali ya mada iliyopita*, na *kuuliza maswali mepesi yanayochokonoa somo jipya*.

Vilevile, watahiniwa wengine walijibu kinyume cha matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika vifaa vya mtaala ambavyo mwalimu anapaswa kuvitumia anapoandaa somo ambavyo ni *muhtasari wa somo, azimio la kazi, andalio la somo* na *vitabu vya kiada na ziada*. Mwingine alibainisha zana zinazoweza kutumika wakati wa kufundisha

aina za maneno (Nomino) kama vile *kadi za maneno, vitu halisi, michoro na picha na hadithi katika matini*. Pia, mtahiniwa mwingine alifafanua vipengele vya andalio la somo huku akihusianisha na mada ndogo ya *Aina za Maneno* ambavyo ni *muda, vitendo vya ufundishaji, ujifunzaji*, na *upimaji*. Mtahiniwa huyo, alitoa majibu hayo kwa sababu andalio la somo huundwa na hatua tano za ufundishaji na ujifunzaji ambapo utangulizi ni hatua mojawapo. Halikadhalika, watahiniwa wengine walieleza hoja moja tu iliyosahihi kati ya nne zilizohitajika na kusababisha kupata alama 0.5 hadi 1. Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa mmojawapo wa kundi hili.



8

i Nomino za kawaida - Arusha, Kilimanjaro, Dodoma

ii Nomino za Pekee - Asha, Juma, Mage.

iii Nomino za dhahania - Mfano Malaika, Mungu, shetani

iv Nomino za jumla - Mfano Mwanajeshi, Wanafunzi


**Kielelezo Na 8.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 8.

Katika kielelezo Na 8.2, mtahiniwa alitaja aina za nomino na mifano yake badala ya kuchambua kwa ufupi mambo manne yanayotakiwa kufanywa na mwalimu katika hatua ya utangulizi wa somo anapofundisha mada ndogo ya *Aina za Maneno* (Nomino).

### 2.1.9 Swali la 9: Uandishi

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kusoma mfano wa hotuba iliyotolewa na Mheshimiwa Makamu wa Rais kisha ajibu maswali katika vipengele vifuatavyo: (a) Kutaja aina ya hotuba; na (b) Kutoa sababu tatu za jibu lake katika (a). Watahiniwa 258 (100%) walijibu swali hili ambapo asilimia 10.5 walipata alama 2 hadi 4. Hivyo, swali hili lilikuwa

miongoni mwa maswali yaliyopata ufaulu hafifu kama inavyoonekana katika Chati Na. 8.




**Chati Na. 8:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 9


Katika chati Na. 8, watahiniwa 231 (89.5%) walipata alama kuanzia 0 hadi 1.5, watahiniwa 17 (6.6%) alama kuanzia 3 hadi 4 na watahiniwa 10 (3.9%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5.

Watahiniwa wengi (89.5%) walipata ufaulu wa kiwango hafifu kutokana na kuwa na uelewa mdogo kuhusu mada ndogo ya *Hotuba*. Hivyo, walishindwa kubainisha aina ya hotuba waliyoisoma katika kipengele (a) na sababu 3 za jibu watakalotoa katika kipengele (b). Wengi wao waliandika kuwa *aina ya hotuba ni hotuba ya tanzia*. Sababu waliyotoa ni kwamba *inatoa taarifa ya kifo, inasikitisha*, na *inawagusa Watanzania* badala ya (a) *Hotuba Kisiasa / Kiserikali* na sababu za kutaja aina hiyo ni kuwa *ilitolewa na kiongozi wa kiserikali, ilitoa taarifa kuhusu kiongozi wa kiserikali, ilihusu shughuli ya kiserikali*, na *ilitolewa katika mandhari yaliyoakisi kuwapo kwa shughuli ya kiserikali*.

Vilevile, watahiniwa wengine waliandika kuwa ni *hotuba rasmi* kwa sababu *imetumia lugha fasaha, haijatumia lugha ya matusi*, na *imetoa taarifa kamili*. Mtahiniwa mwingine aliandika kuwa ni *hotuba sahihi* kwa sababu *imetumia mtiririko sahihi kwa kuanza na kichwa cha hotuba, utangulizi, kiini na hitimisho*. Watahiniwa hawa, walishindwa kutambua kwamba kuna sifa za jumla za hotuba na sifa mahususi

kulingana na aina husika. Kwa mfano, unapoandika hotuba za shuleni zina sifa mahsusi tofauti na hotuba za kiserikali. Watahiniwa hawa waliandika aina tofauti tofauti za hotuba na sifa zake ambazo hazikuwa sahihi kutokana na uelewa mdogo wa kutumia mazingira ya hotuba husika katika kubainisha aina mahsusi.

Aidha, mtahiniwa mwingine aliweza kutaja aina ya hotuba na kushindwa kutaja sababu tatu za kutaja aina hiyo. Hivyo, watahiniwa hawa walipata alama 1. Majibu ya mtahiniwa huyo yalikuwa: *Ni hotuba ya Kiserikali kwa sababu inatoa taarifa ya msiba, inahusu kuondokewa na jemedari,* na *inahusu majonzi ya taifa.* Kwa ujumla, watahiniwa hao walishindwa kubaini sifa za hotuba ya kiserikali/kisisasa badala yake wakajikita kwenye maudhui ya tanzia yaliyokuwa yameoneshwa katika hotuba hiyo. Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



9
i) Hotuba ya nchi
ii) a) Ni hotuba ya nchi kwasababu Rais Dkt. John pombe magufuli alikuwa ni Rais wa Jamuhuri ya muungano wa Tanzania.
b) Ni hotuba ya nchi kwasababu ilitolewa na Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya muunga no wa Tanzania.
c) Ni hotuba ya nchi kwasababu Makamu wa Rahis alifanya hotuba hiyo akiwa nchi ya Tanzania.

**Kielelezo Na. 9.1:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 9.

Kielelezo Na. 9.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyebainisha aina ya hotuba kuwa ni hotuba ya nchi na sifa zake badala ya hotuba ya kiserikali/kisiasa na sifa zake. Mtahiniwa huyu, aliandika majibu hayo kwa sababu ya uhusiano uliopo kati ya serikali na nchi kwa kuwa serikali ni chombo kinachoendesha nchi. Hivyo, uhusiano huo ulimfanya mtahiniwa kuona kuwa aina hiyo ya hotuba ni hotuba ya nchi na kutaja sifa zake.

Vilevile, asilimia 6.6 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata kiwango kizuri cha ufaulu. Waliweza kutaja aina ya hotuba kwa usahihi

katika kipengele (a) na kubainisha sababu tatu za kutaja aina hiyo katika kipengele (b). Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa: (a) *Ni hotuba ya kiserikali, na (b) Inatolewa na kiongozi wa kiserikali ambaye ni Makamu wa Rais, ilitoa taarifa kuhusu kiongozi wa kiserikali na ilihusu shughuli ya kiserikali.* Kielelezo Na.9.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa mmojawapo katika kundi hili.


9 (a) Hotuba ya kisiasa
(b)(i) Aliyeitwa alikuwa ni makamu wa rais ni kama mwanasiasa.
(ii) Hotuba pia ilikuwa inalenga kicho cha mwanasiasa ambaye ni rais pia.
(iii) Hotuba ilikuwa inawaruhusu watanzania wote.


**Kielelezo Na. 9.2:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 9.

Kielelezo Na. 9.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu swali kwa usahihi ingawa hoja ya (iii) haikuwa sahihi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa wachache (3.5%) walipata ufaulu wa kiwango cha wastani katika swali hili kwa kuwa waliweza kutaja aina ya hotuba katika kipengele (a) na sababu moja kati ya tatu katika kipengele (b). Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu kama ifuatavyo: (a) *Ni hotuba ya Kiserikali* kwa sababu *ilitolewa na kiongozi wa serikali, huzingatia ukweli wa jambo na hutumia lugha rasmi*. Mtahiniwa huyu aliandika sababu sahihi kuwa *ilitolewa na kiongozi wa serikali* ila sababu ya *kuzingatia ukweli wa jambo na kutumia lugha rasmi* hazikuwa sahihi kwani ni sifa za jumla zinazotakiwa kuzingatiwa katika uandishi wa hotuba ya aina yoyote. Hii inadhihirisha kuwa watahiniwa wa kundi hili walikuwa na uelewa wa wastani juu ya aina za hotuba na sifa zake.

### 2.1.10 Swali la 10: Upimaji


Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi aina nne za upimaji atakazotumia ili kujua maendeleo ya wanafunzi wake kitaaluma. Watahiniwa 258 (100%) walifanya swali hili. Swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwani asilimia 77.9 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4. Hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kama inavyoonekana katika Chati Na. 9.




**Chati Na. 9:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 10*

Chati Na. 9 inaonesha kuwa watahiniwa 198 (76.7%) walipata alama kuanzia 3 hadi 4, watahiniwa 57 (22.1%) alama kuanzia 0 hadi 1.5 na watahiniwa 3 (1.2%) walipata alama kuanzia 2 hadi 2.5.

Watahiniwa wengi (76.7%) walijibu swali hili kwa usahihi. Waliweza kuelezea aina 3 hadi 4 za upimaji wanazoweza kutumia ili kujua maendeleo ya kitaaluma ya wanafunzi wao. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza aina zifuatazo kwa usahihi: *upimaji wa awali ambao hufanyika kabla ya kuanza masomo au mada fulani*, *upimaji gunduzi ambao mwalimu huufanya anapokuta mwanafunzi wake ana tatizo fulani katika kujifunza*, *upimaji endelezi ambao hufanywa wakati wowote kadri mwalimu anavyoendelea kufundisha mada zake*, na *upimaji tamati ambao unaofanywa mwishoni mwa mafunzo fulani.* Kielelezo Na.10.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



10
(i) Upimaji wa awali
Hufanyika kabla ya kuanza mafunzo/kozi fulani.
Mwalimu humpima mwanafunzi ili kujua ujuzi alio nao mwanafunzi katika mada/kozi fulani.
(ii) Upimaji endelevu.
Huu ni upimaji ambao hufanyika ndani ya mafunzo yakiendelea
(iii) Upimaji tatuzi/gunduzi. Hufanyika pale mwalimu anapobaini kuna tatizo ili kutafuta utatuzi wa tatizo hilo
(iv) Upimaji tamati- Hufanyika mwishoni mwa kozi/mafunzo fulani ili kutunuku cheti au kuvusha darasa moja kwenda lingine

**Kielelezo Na.10.1:** Sampuli ya majibu sahihi katika swali la 10.

Hata hivyo, asilimia 22.1 ya watahiniwa walishindwa kuelezea aina nne za upimaji wanazoweza kutumia ili kujua maendeleo ya kitaaluma ya wanafunzi wao hivyo, kupata alama 0 hadi 1.5. Watahiniwa hawa, walikuwa na uelewa mdogo juu ya mada ndogo ya *Kutunga Maswali*. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *upimaji wa papo kwa papo, upimaji wa muda mrefu, upimaji mkubwa*, na *upimaji wa kati* badala ya *upimaji wa awali ambao hufanyika kabla ya kuanza masomo au mada fulani*, *upimaji gunduzi ambao mwalimu huufanya anapokuta mwanafunzi wake ana tatizo fulani katika kujifunza*, *upimaji endelezi ambao hufanywa wakati wowote kadri mwalimu anavyoendelea kufundisha mada zake* na *upimaji tamati ambao unaofanywa mwishoni mwa mafunzo fulani*. Aidha, mtahiniwa mwingine alibainisha wadau wanaohusika kufanya ufuatiliaji kutokana na matokeo ya upimaji wa wanafunzi. Mtahiniwa huyo aliandika: *upimaji kwa mwalimu, mwanafunzi, shule na taasisi za elimu*.

Pamoja na hayo, watahiniwa wengine wa kundi hili hawakuelewa matakwa ya swali. Mathalani, mtahiniwa mmojawapo aliandika umuhimu wa upimaji badala ya aina nne za upimaji na mwingine alitaja nyanja za upimaji ambazo ni *kukumbuka, kufahamu, kutumia*, na *kutathmini.* Aidha, mtahiniwa mwingine alifafanua mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ambazo ni: *bungua bongo, majadiliano ya vikundi, matembezi ya galare*, *na fikiri kijozi*. Watahiniwa hawa walitoa majibu hayo kwa sababu mwalimu huzingatia nyanja za upimaji anapoandaa maswali mbalimbali ya upimaji na upimaji ni shughuli inayojumuishwa

katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Jambo lililosababisha watahiniwa hawa kufafanua nyanja za upimaji na mbinu za kufundishia na kujifunzia Kiswahili mtawalia. Aidha, watahiniwa wengine walifanikiwa kueleza aina moja kati ya nne na wengine walitaja aina tatu bila kuelezea kama yalivyokuwa matakwa ya swali. Kielelezo Na.10.2 Kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kueleza aina nne za upimaji.



10

i) Mazoezi ya darasani, Mwalimu anaweza kuwapima wanafunzi kitaaluma kwa kuwapa mazoezi mbalimbali kutoka katika mada alizofundisha

ii) Majaribio, kuwapima kwa kuwa majaribio ya wiki au mwezi kupitia mada walizojifunza.

iii) Mitihani, Mwalimu anaweza kuwapima wanafunzi kwa kuwapa mitihani iliyotungwa kwa kufuata utaratibu wa upimaji Mitihani inaweza kuwa ya robo muhula, au nusu muhula.

iv) Kazi za vikundi, Mwalimu anaweza kuwaandalia wanafunzi maswali ya kujibu kwa vikundi.

**Kielelezo Na.10.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 10.


Katika kielelezo Na. 10.2, mtahiniwa alishindwa kuelezea kwa ufupi aina za upimaji anazoweza kutumia kujua maendeleo ya kitaaluma ya wanafunzi wake badala yake alielezea zana za upimaji.

## 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha

Sehemu hii ilikuwa na maswali manne (4) ya insha ambayo yalitungwa kutoka katika mada ya *Taaluma ya Kiswahili* na *Utaalamu wa Kufundisha Kiswahili*. Mtahiniwa alipaswa kujibu maswali yote ambapo kila swali lilikuwa na alama kumi na tano (15). Hivyo, kufanya sehemu hii kuwa na jumla ya alama sitini (60). Aidha, ufaulu wa watahiniwa katika sehemu hii umegawanyika katika makundi matatu. Mtahiniwa alibainishwa kuwa na kiwango hafifu cha ufaulu endapo alipata alama kuanzia 0 hadi 5.5, wastani endapo alipata alama kuanzia 6 hadi 10 na alihesabika kuwa na kiwango kizuri iwapo alipata alama 10.5 hadi 15.

### 2.2.1 Swali la 11: Uhakiki wa Kazi za Fasihi

Swali lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha kwa kutumia hoja tano kuwa mhakiki ana mchango mkubwa katika uchambuzi wa kazi za kifasihi. Watahiniwa 258 (100%) walijibu swali hili. Miongoni mwao, asilimia 93.8 walipata alama 6 hadi 15. Hivyo, swali lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri. Chati Na.10 inaonesha mchanganuo wa ufaulu wa watahiniwa.




**Chati Na. 10:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 11

Chati Na. 10 inaonesha kuwa watahiniwa 193 (74.8%) walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15, watahiniwa 49 (19.0%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na watahiniwa 16 (6.2%) walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5.

Katika chati Na.10, watahiniwa zaidi ya nusu (74.8) walijibu vizuri swali hili. Watahiniwa hawa, walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa mhakiki wa kazi mbalimbali za kifasihi. Hivyo, waliweza kuthibitisha kuwa mhakiki ana mchango mkubwa katika uchambuzi wa kazi za kifasihi kwa hoja 4 hadi 5. Aidha, waliweza kuelezea hoja zao, kuandika sehemu ya utangulizi na hitimisho linaloendana na swali. Miongoni mwa majibu yao ni: *Huchambua na kuweka wazi funzo ambalo linatolewa na kazi ya fasihi*, *Huchambua na kufafanua picha za kisanii zilizotumika katika kazi ya fasihi*, *Humshauri mwandishi ili*

*afanye kazi bora zaidi*, *Humuelekeza msomaji ili apate faida zaidi kuliko yale ambayo angeweza kuyapata bila dira ya mhakiki*, *Husema ukweli ipasavyo kuhusu tamaduni na falsafa zinazotawala fasihi*, *hili pia ni jukumu la mhakiki baada ya kuichambua kazi husika ataeleza tamaduni zinazotawala jamii* na *Kuheshimu na kuthamini kazi ya mwandishi kwa kuzifanyia haki*. Kielelezo Na.11.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

11

Mhakiki, Ni mtu anayechambua na kuhakikisha kazi ya msanii ili iweze kuwasilishwa katika jamii yake. Mhakiki ni mtu pia anayerahisisha kazi ya fasihi iweze kueleweka katika jamii kwa sababu inatumia lugha ya picha, utata na tamathali za semi zinazopelekea kuifanya kazi ya fasihi isieleweke kwa urahisi. Kwa maana hiyo mhakiki ana mchango mkubwa katika uchambuzi wa kazi za fasihi (zifuatazo ni miongoni mwa mchango katika uchambuzi wa kazi za kifasihi kama vile:-

Kurahisisha kazi ya fasihi iweze kueleweka kiurahisi, wasanii wengi watumia lugha ya mficho ambayo ni ngumu kuelewa kwa urahisi lakni kwa kutumia uhakiki wa kazi hiyo tunaweza kuelewa zaidi maana ya kile alichokuwa akikiongelea kwa urahisi zaidi

Kuweka wazi mambo yanayoikumba jamii yetu, Mhakiki anasaidia sana katika kufumbua mafumbo anayotumia msanii na mhakiki anayaweka wazi ili jamii iweze kutambua jinsi jamii yetu ilivyo mfano tukiangalia katika kitabu cha "Mwalimu Rozi" tunamuona Mwalimu Rozi alivyokuwa na tabia mbaya ambayo aziyoi kuigwa na jamii kama vile ulevi, ukahaba na uasherati kutokana na dhana hiyo mhakiki anamuelezea vizuri Mwalimu Rozi kwa lugha nyepesi kabisa na kusababisha jamii kuelewa nini kinaendelea

Humsaidia mwanafunzi kujua na kuelewa matumizi ya lugha, Hapa mwanafunzi anaelewa kwa uhaaka zaidi matumizi ya lugha kuliko kuenye

11 Cont.

kitabu au kazi ya msanii mwenyewe kwa sababu mhakiki anatofautisha aina za matumizi ya lugha mfano kitabu cha Ngoma ya Ng'wana Malundi kuna matumizi ya taswira kama jina la kitabu lenyewe mhakiki anasema ni ishu ya kujikomboa.

Anachambua kwa kina zaidi kuhusu kazi ya msanii, Msanii anapoitunga kazi yake humpa mhakiki wake ili kuhakikisha kazi yake inakaa sawa hivyo msanii bila mhakiki haipendezi kwa sababu mhakiki anachambua zaidi kwa kina kazi ya msanii hukuika

Husaidia kukuza vipaji vya waandishi, Mhakiki ana mchango mkubwa katika uchambuzi wa kazi ya fasihi kwa sababu husaidia kukuza na kuboresha vipaji vya waandishi na kusababisha kuandaa wasanii bora, wenye vigezo, na wanaohitajika katika jamii ili kuhakikisha kazi inayozalishwa katika jamii ni bora na yenye kufaa kuigwa na jamii, badala yake wayaishi mazuri na mabaya waachane nayo kama vile ulevi uliokithiri katika riwaya ya Ua la Faraja.

Husaidia kutoa kazi yenye ubora, Msanii anapoandika kazi yake inakuwa haina ubora zaidi na hivyo ili iwe bora inatakiwa kuhakikiwa na kusambazwa katika jamii hii inasababisha endapo kazi haitahakikiwa itapotosha watu na kuendelea kudidimiza nchi yetu hivyo ili fasihi iendelee kuishi,

**Kielelezo Na.11.1:** Sampuli ya sehemu ya majibu sahihi katika swali la 11.

Vilevile, baadhi ya watahiniwa (19.0%) walipata alama za wastani kutokana na kuwa na uelewa wa wastani waliokuwa nao juu ya umuhimu wa mhakiki wa kazi za kifasihi. Hivyo, walithibitisha kuwa mhakiki wa kazi za kifasihi ana mchango mkubwa katika uchambuzi wa kazi za kifasihi kwa kuelezea hoja 2 hadi 3 pamoja na kuandika sehemu ya utangulizi na hitimisho lisiloendana na swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alieleza hoja 2 sahihi ambazo ni *mhakiki husaidia kuchambua vipengele vya fani na maudhui na kuboresha kazi za fasihi*. Aidha, alitoa hoja 3 zisizo sahihi zinazofafanua sifa za mhakiki ambazo ni kuwa *lazima aelewe tamaduni za jamii anayoichambulia kazi husika, lugha fasaha*, na *nadharia mbalimbali za uhakiki.* Aidha, aliandika kwa usahihi sehemu ya utangulizi lakini alishindwa kuandika hitimisho linaloendana na swali. Pia, mtahiniwa mwingine aliandika hoja tatu kati ya tano tofauti na yalivyokuwa matakwa ya swali hivyo, kusababisha kupata alama za wastani.

Hata hivyo, wapo watahiniwa waliopata alama kuanzia 0 hadi 5.5 ambao ni sawa na asilimia 6.2. Watahiniwa hawa, walikuwa na uelewa mdogo kuhusiana na umuhimu wa mhakiki katika uchambuzi wa kazi za kifasihi. Hivyo, walishindwa kuthibitisha kuwa mhakiki ana mchango mkubwa katika uchambuzi wa kazi za kifasihi. Baadhi yao, waliandika hoja dhaifu ambazo haziwezi kuthibitisha mchango wa mhakiki katika uchambuzi wa kazi za kifasihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kuwa *mhakiki humuunganisha mwandishi na jamii, humwasilisha katika jamii, humtambulisha, Humpa nafasi ya kuheshimiwa na Humuunganisha na waandishi wengine*. Hata hivyo, aliandika sehemu ya utangulizi kwa usahihi na kusababisha kupata alama 1. Aidha, watahiniwa wengine walifanikiwa kuelezea hoja mbili tu sahihi kati ya tano na wengine kutaja hoja zote kwa usahihi bila kueleza hivyo walipata alama hafifu.

Vilevile, watahiniwa wengine walijibu kinyume cha matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichambua dhamira tano zinazojitokeza katika kazi mbalimbali za kifasihi kama vile *rushwa, uongozi mbaya, imani potofu, ukatili wa kijinsia*, na *ulevi*, na mwingine alichambua vipengele vya fani kama vinavyotumika na msanii katika kusuka kazi za kifasihi ambavyo ni *muundo, mtindo, wahusika, mandhari*, na *jina na jalada la kitabu*. Kadhalika, mtahiniwa mwingine alifafanua kazi za kifasihi zinazochambuliwa na mhakiki ambazo ni *tamthiliya, riwaya*, na

*ushairi*. Watahiniwa hawa, walishindwa kutambua kuwa swali halikuhitaji vipengele wala kazi mbalimbali zinazochambuliwa na mhakiki bali lilihitaji kuelezea hoja zinazothibitisha mchango mkubwa alionao mhakiki katika kufanya kazi ya uchambuzi wa kazi za kifasihi. Kielelezo Na.11.2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa ambaye hakuweza kubainisha mchango wa mhakiki katika kazi za fasihi.

11

Mhakiki: Ni Mtu anayejishughulisha na uchambuzi wa kazi za Fasihi. Mhakiki anaweza kufanya ~~u~~ uchambuzi katika maeneo mawili ambayo ni katika Maudhui na Fani. Maudhui umbo la nje la kazi ya Fasihi na Fani ni umbo la ndani la kazi ya fasihi. Mhakiki anamchango mkubwa katika uchambuzi wa kazi za Fasihi kwa kutumia hoja zifuatazo.

Maudhui ni umbo la nje la kazi za Fasihi

Mhakiki anaweza kuchambua mambo yafuatayo.

Dhamira - Ni kiini cha kazi za Fasihi au Funzo tunalolipata katika kazi za fasihi. Mfano katika riwaya ya Ua la Faraja tunapata dhamira mbalimbali mfano Madhara ya Ukimwi hivyo mhakiki anafanya kazi ya kuchambua vipengele vya kila kazi ya Fasihi.

Ujumbe - Ni mafunzo na maadili tunayoyapata katika uchambuzi wa kazi za Fasihi mfano katika kazi mbalimbali za Fasihi tunapata mafunzo mbalimbali katika kazi za fasihi mfano katika Tamthilia ya Mwalimu Rosa tunapata ujumbe kuwa matumizi mabaya ya madaraka ni chanzo cha maendeleo duni katika jamii.


Falsafa - Falsafa ni Imani ya Mwandishi au imani nyingine katika kazi za Fasihi Mhakiki ana kazi ya kuchambua Falsafa za waandishi katika kazi za Fasihi mfano katika Tamthilia ya Mwalimu Rosa Mwandishi anasema

**Kielelezo Na.11.2:** Sampuli ya sehemu ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 11.

Kielelezo Na. 11.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyefafanua vipengele vya maudhui badala ya kuelezea mchango wa mhakiki katika uchambuzi wa kazi za kifasihi.

### 2.2.2 Swali la 12: Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kufafanua miundo sita ambayo kikundi nomino kinaweza kujidhihirisha na kutoa mifano miwili kwa kila muundo. Watahiniwa 258 (100%) walijibu swali hili ambapo asilimia 77.5 walipata alama 6 hadi 15. Hivyo, swali hili lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri kama inavyoonekana katika chati Na. 11.




**Chati Na. 11:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 12

Chati Na. 11 inaonesha kuwa, watahiniwa 123 (47.7%) walipata alama 10.5 hadi 15, 77 (29.8%) alama 6 hadi 10 na watahiniwa 58 (22.5%) walipata alama 0 hadi 5.5.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, asilimia 47.7 ya watahiniwa waliojibu swali hili, walijibu vizuri. Hawa walikuwa na uelewa wa kutosha waliokuwa nao kuhusu miundo ya tungo mbalimbali za Kiswahili. Hivyo, waliweza kufafanua miundo 4 hadi 6 ambayo kikundi

nomino huweza kujidhihirisha na kutoa mifano miwili katika kila muundo. Miongoni mwa majibu yaliyoandikwa na watahiniwa wa kundi hili ni kama ifuatavyo: *(i) muundo wa umbo kapa (Ө). Hili ni umbo ambalo halidhihiriki katika muundo wa nje. Huwa katika muundo wa ndani tu. Kwa mfano, Hukumwona Subira? (Wewe) hukumwona Subira? Na Vilivyopotea vimepatikana? (Vitu) vilivyopotea vimepatikana (ii) Nomino pekee. Wakati mwingine kikundi nomino huwa na nomino pekee. Kwa mfano, Meli imewasili ufuoni* au *Nguo imechanika vibaya*; *(iii) Kiwakilishi pekee. Wakati mwingine*, *kikundi nomino huwa na kiwakilishi pekee. Kwa mfano*, *Wao watafika kesho asubuhi au Hilo lilimfurahisha mno; (iv) Nomino na Kivumishi: Wakati mwingine kikundi nomino huwa ni kiwakilishi na kivumishi chake. Kwa mfano, Wakulima hodari wanavuna mazao shambani ambapo wakulima- N, V – hodari na Wanafunzi wengi walifeli mitihani - wanafunzi, V – wengi*; *(v) Kiwakilishi na kivumishi. Wakati mwingine kikundi nomini huwa na kiwakilishi na kivumishi chake. Kwa mfano: Vile vyote vililetwa jana. Neno vile ni kiwakilishi,* na *vyote ni kivumishi.* Katika sentensi *Zile chache ziacheni kwanza*, *neno zile ni kiwakilishi na chache ni kivumishi*; *(vi) Nomino na kirai vumishi. Wakati mwingine*, *kikundi nomino huwa ni nomino na kirai vumishi. Kwa mfano; Ng'ombe huyu wangu ni mweusi? Ng'ombe- ni nomino na huyu wangu ni kirai kivumishi au Magunia yenye sukari, yalipakiwa humo ambapo Magunia ni nomino na yenye sukari ni kirai kivumishi*; na *(vii)Nomino na Kirai kihusishi. Wakati mwingine kikundi nomino huwa ni nomino na kirai kihusishi. Kwa mfano, Mguu wa ng'ombe huwa na kwato ambapo mguu ni nomino na wa ng'ombe ni kirai kihisishi au Chai ya maziwa ni tamu ambapo chai ni nomino, ya maziwa ni kirai kihisishi*. Kielelezo Na.12.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubainisha miundo sahihi ya kikundi nomino.

12

Nomino. Ni aina za maneno ambayo ni majina ya watu, wanyama na vitu. Kikundi Nomino Ni aina ya kirai ambayo hukaa kabla ya kitenzi. Katika kikundi nomino kuna aina nyingi za maneno ambayo yanapatikana katika kikundi nomino. Ifuatayo ni miundo ya kikundi nomino.

Nomino peke yake (N). Hii ni muundo wa kikundi nomino ambao inakuwa peke yake (inakuwa nomino moja) kabla ya kitenzi. Hivyo kikundi nomino huundwa na Nomino moja tu. Mfano: Mtoto anacheza. mpira. Kwahiyo kikundi nomino huundwa na nomino moja. - Juma anakimbia.

Nomino na Nomino (N+N). Hii ni muundo wa kikundi nomino ambao huundwa na Nomino mbili (Nomino na Nomino (N+N)). Mfano: - Baba na Mama wanalima. Kwahiyo Kikundi Nomino (KN) huundwa na Nomino mbili au zaidi (N+N). - Juma na Asha wanasoma.

Nomino na Kivumishi (N+V). Hii pia ni kikundi Nomino (KN) ambacho huundwa na Nomino na kivumishi (N+V) katika sentensi. Mfano: - Watoto wangapi wanaimba? Kwahiyo Kikundi Nomino (KN) huundwa na Nomino na kivumishi. Mfano: - Wanafunzi wanne wametoroka.

Kiwakilishi na Kivumishi. Kikundi Nomino (KN) huundwa na kiwakilishi na kivumishi. Katika sentensi kuna kiwakilishi pia kivumishi. Mfano: - Wale watano wanacheza

12 Cont.

- Yule mwizi amekamatwa. Kwahiyo kikundi Nomino huundwa na kivumishi na kiwakilishi katika sentensi.

Nomino na Kishazi tegemezi. Kikundi Nomino katika sentensi huundwa na nomino na kishazi tegemezi mfano: - Mtoto aliyepotea jana amepatikana. - Mwizi aliyeimba juzi amekamatwa. Kwahiyo kikundi Nomino huundwa na Nomino moja na kishazi tegemezi (N + BV).

Kiwakilishi peke yake (W). Katika kikundi Nomino, kiwakilishi kinaundwa peke yake katika sentensi kabla ya kitenzi. Mfano: - Wangapi wameandika? - Wangapi wamepika. Kwahiyo, kikundi nomino (KN) kimeundwa na kiwakilishi peke ake katika sentensi.

Kwahiyo. Kikundi Nomino ni kikundi kirai. Kikundi kirai ni maneno yote ambayo hayana muundo wa kiima na kiarifu. Pia kikundi kirai huwa upande wa kiima.


**Kielelezo Na.12.1:** Sampuli ya sehemu ya majibu sahihi katika swali la 12.

Vilevile, asilimia 29.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa wastani kuhusu miundo mbalimbali ya kikundi nomino (KN). Hivyo, waliandika miundo 3 hadi 4 kati ya 6 kwa usahihi na kushindwa kuandika sehemu ya utangulizi na hitimisho sahihi. Aidha, wengine waliandika miundo sahihi na isiyo sahihi kutokana na kuchanganya dhana ya kikundi nomino na aina za nomino. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika miundo mitatu sahihi ambayo ni *muundo wa nomino pekee; nomino na kivumishi;* na *kiwakilishi na kivumishi*, na miundo isiyosahihi ambayo ni: *nomino dhahania, nomino za pekee na nomino jumuishi*. Hivyo, kusababisha kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, asilimia 22.5 ya watahiniwa walipata alama hafifu kutokana na uelewa mdogo kuhusiana na miundo ya kikundi nomino. Miongoni mwao, waliandika miundo ambayo kikundi nomino hakiwezi kujidhihirishi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *muundo wa chagizo*, *muundo wa kielezi*, *muundo wa kitenzi*, *muundo wa kiima na kiarifu* badala ya *muundo wa nomino pekee, muundo kapa, kiwakilishi pekee, kiwakilishi na kivumishi, nomino na kishazi tegemezi na nomino na kirai kihusishi*. Hii inadhihirisha kuwa mtahiniwa huyu hak uelewa kuwa kikundi nomino hakiwezi kuundwa na kielezi wala kitenzi kwa sababu hizo ni aina za maneno ambazo hukaa upande wa kiarifu wa sentensi ilihali kikundi nomino mara nyingi hukaa upande wa kiima. Aidha, kielezi huunda kikundi kielezi na kitenzi huunda kikundi kitenzi. Pia, muundo wa kiima na kiarifu sio miundo ya kikundi nomino bali ni sehemu kuu mbili za sentensi.

Kadhalika, watahiniwa wengine walitunga sentensi sita zenye aina mbalimbali za nomino na kubainisha nomino hizo kuwa ndio miundo ya kikundi nomino. Miongoni mwa majibu ya watahiniwa hao ni kama vile: *<u>Juma</u> anakwenda shuleni; Asha anaishi <u>Dodoma</u>; <u>Mungu</u> ni mkubwa; <u>Upepo</u> umevuma sana; <u>Wanajeshi</u> wamerudi kambini;* na *<u>Maziwa</u> yamemwagika.* Watahiniwa hao walibainisha maneno yaliyopigiwa mstari kuwa ndio miundo ya kikundi nomino. Kwa ujumla, walifikiri kwamba kikundi nomino hakiwezi kuundwa na aina nyingine za maneno kama vile kiwakilishi na kivumishi.

Pia, kuna watahiniwa wengine walieleza maana ya nomino katika hoja sita. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *nomino hutaja majina ya pekee, majina ya vitu, majina ya watu, mahali au miji* na *vitu vinavyoonekana au visivyoonekana*. Wengine walifafanua miundo ya silabi ambayo ni: *Irabu pekee, Konsonanti pekee, Konsonanti + irabu, konsonanti+ konsonanti+ irabu na konsonanti+ konsonanti+ irabu*. Pamoja na hayo, watahiniwa wengine walifanikiwa kuandika muundo sahihi mmoja kati ya sita na sehemu ya utangulizi hivyo, kusababisha kupata alama hafifu. Kielelezo Na.12.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa ambaye hakuweza kubainisha namna kikundi nomino kinavyoweza kujidhihirisha katika miundo mbalimbali.


12

Kikundi nomino; Ni kikundi cha maneno ambacho hutaja majina ya vitu kama watu, wanyama na mimea. Kikundi nomino kina miundo mbalimbali ambayo hutumika katika mazingira tofauti tofauti. Ifuatayo ni miundo ya kikundi nomino nayo ni:-

Nomino za kawaida; Hizi ni aina za nomino ambazo hutaja majina ya kawaida. Mfano John, Asha, Tembo na Sungura. Nomino hizi mara nyingi hutaja majina ya kawaida ambayo humfahamisha mtu au mnyama au mahali.

Nomino za jumla; Ni aina za nomino ambazo hutaja majina ya jumla na huwatambulisha wao ni kani. Mfano Bunge, wanajeshi na majina mengine ya jumla. Nomino hizi husaidia kutambulisha watu kwa umoja au kwa pamoja wao wanajulikanaje.

Nomino za dhahania; Mfano Njaa, Mungu, majini na vitu vingine vingi ambavyo ni vyakudhani. Nomino hizi hutaja vitu ambavyo havionekani na havishikiki hivyo huvitambulisha au hujulikana kama ni kikundi nomino dhahania.

Nomino za idadi; Hizi ni aina za nomino ambazo hutaja idadi ya vitu au watu kuwa wapo wangapi au vipo vingapi. Mfano watatu waje mbele, vinne vile pale. Hapo nomino hizi za idadi zinaonesha kuwa vitu hivyo au watu hao wapo wangapi na wanahitaika.

12 Cont.

Nomino za pekee; Hizi ni aina za nomino ambazo huonesha upekee ndani yake na humuelezea sifa za mtu kuwa yeye yupoje. Mfano wa nomino za pekee ni Juma ndiye hodari, Amina amefaulu peke yake darasani. Hivyo nomino hizi za pekee zinatoa sifa za mtu aliyetenda jambo fulani.

Nomino za jina kwa jina; Ni nomino ambazo huambatanisha majina ya vitu au watu katika sentensi moja. Mfano Aisha na Baraka ni watoto wapole sana, Fisi na mbuzi hawawezi kukaa zizi moja. Hivyo nomino hizi zinakuwa zimeambatana katika sentensi moja na kukamilisha maana bila kupoteza uhalisia wa sentensi.

Hitimisho, katika aina za maneno nomino au kikundi nomino mara nyingi hujikita katika kutaja majina ya vitu, watu, wanyama na mahali hivyo kikundi nomino mara nyingi ndio hukamilisha sentensi, na husaidia kujua majina tofauti tofauti ya vitu kijumla, kiidadi na kipekee.

**Kielelezo Na.12.2:** Sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 12.

Kielelezo Na. 12.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kuelezea miundo sita ambayo kikundi nomino huweza kujidhihirisha badala yake alielezea aina mbalimbali za nomino.

### 2.2.3 Swali la 13: Upimaji

Mtahiniwa alitakiwa kuelezea misingi mitano atakayozingatia wakati wa utunzi wa maswali ya majibu mafupi. Watahiniwa 258 (100%) walijibu swali hili ambapo asilimia 0.8 tu ndio waliopata kiwango cha wastani. Hivyo, kufanya swali hili kuwa miongoni mwa maswali yenye kiwango hafifu cha ufaulu kama inavyoonekana katika Jedwali Na.2.

**Jedwali Na. 2:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 13


| Na | Alama | Idadi ya Watahiniwa | Asilimia ya Watahiniwa |
|---|---|---|---|
| 2. | 6 – 10 | 2 | 0.8 |
| 3. | 0-5.5 | 256 | 99.2 |

Katika jedwali Na. 2, watahiniwa 256 (99.2%) walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5 na watahiniwa 2 (0.8%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10. Hata hivyo, hakukuwa na watahiniwa waliopata alama kuanzia 10 hadi 15.

Jedwali Na. 2 linaonesha kuwa, watahiniwa wengi (99.2%) walishindwa kujibu swali hili kwa usahihi. Hii ilitokana na uelewa mdogo waliokuwa nao katika mada ndogo ya *Aina za Maswali*. Hivyo, walishindwa kuelezea misingi mitano ya kuzingatia wakati wa kutunga maswali ya majibu mafupi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika misingi ya jumla ya kuzingatia katika utunzi wa maswali ya aina yoyote kama vile *kutumia lugha inayoeleweka, kutokutumia lugha yenye utata, kuzingatia mada zilizofundishwa, mahitaji ya wanafunzi na ngazi ya wanafunzi husika* badala ya kuandika misingi mahsusi ya kuzingatia wakati wa utunzi wa maswali ya majibu mafupi ambayo ni *kuliza maswali ambayo majibu yake ni mafupi, wazi na bayana; kutokuchukua sentensi moja kwa moja kutoka kwenye kitabu kama shina la swali; kutumia mtindo wa swali la kawaida zaidi kuliko kutumia mtindo wa kujaza nafasi zilizoachwa wazi; Kama swali linahitaji kutoa vipimo fulani basi onesha wazi kuwa ni vipimo gani vitatumika au kama kuna maelekezo mahsusi*

*ya njia ya kufanya swali hilo inashauriwa mwanafunzi kuwekwa bayana;* na *iwapo mtindo uliotumika ni wa kuacha nafasi wazi ili mwanafunzi ajaze majibu, nafasi hizo zinapaswa kuwa na urefu unaolingana*.

Pia, watahiniwa wengine hawakuelewa matakwa ya swali. Mathalani, mtahiniwa mmojawapo alielezea misingi ya kujifunza Kiswahili ambayo ni *msingi wa kusikiliza*, *kuzungumza*, *kuandika*, *kusoma, kujieleza na msingi wa kutumia lugha za kisanaa*. Halikadhalika, watahiniwa wengine waliandika mambo ya kuzingatia katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kama vile *uelewa wa wanafunzi, mada husika, wingi/ukubwa wa darasa, muda* na *muhtasari wa somo*. Kwa ujumla, watahiniwa hawa walichanganya mambo ya kuzingatia katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji na misingi ya kuzingatia wakati wa utunzi wa maswali ya majibu mafupi. Hii imesababishwa na dhana ya utunzi wa maswali kupatikana katika mada ya upimaji na upimaji pia ni kitendo kinachofanyika katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Vilevile, watahiniwa wengine walifanikiwa kuelezea msingi mmoja sahihi kati ya mitano na kushindwa kuandika kwa usahihi sehemu ya utangulizi na hitimisho linaloendana na matakwa ya swali hivyo, kupata alama hafifu. Kielelezo Na. 13.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu vibaya swali hili na kupata alama 0.


13

Upimaji ni kitendo cha kuandaa maswali kwa mtu au Mwanafunzi anayeandaliwa kwenda - kiwango kingine cha elimu, kwa maandalizi sahihi. Zifuatazo ni hatua muhimu ya kufuata wakati wa kuandaa Maswali ya upimaji, kama ifuatavyo:-

Kufahamu Kiwango cha elimu ya mwanafunzi hii ni kuelewa ufaulu wa mwanafunzi darasani kwani Mwanafunzi ambaye hajaelewa vizuri huwezi kumtolea Maswali magumu kwa lengo la kumwandaa kufemkwa katika kiwango chake cha elimu.

Lazima Mwalimu afahamu mada - zilizofundishwa na wanafunzi kuelewe kwa kiwango fulani darasani baada ya kuona wanafunzi zaidi ya 50% wameelewa mada hiyo ambayo unataka kutungia Maswali ya upimaji wa Maendeleo ya wanafunzi wa kidato cha kwanza

Lazima Mwalimu afahamu jumla ya mada ambayo anataka kutunga katika mtihani huo Hii husaidia Mwalimu kujue kutunga - Maswali kadaa kwa kila mada Mfano aina za Maneno na Mengine kama vile fasihi . kwa ujumla, na Sarufi ya kiswahili.

Mwalimu lazima ajue idadi ya vipindi kwa Mada kuu na mada ndogo hii husaidia Mwalimu kuandaa Maswali ambayo anahitaji kuyatunga vile vile kujua jumla ya Maswali yote ili yaweze kumsaidia katika kukokotoa jumla ya maswali ya kila mada inayohusika

**Kielelezo 13.1:** Sampuli ya sehemu ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 13.


Kielelezo Na. 13.1 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyefafanua mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa jedwali la utahini badala ya mambo ya kuzingatia wakati wa utunzi wa maswali ya majibu mafupi.

Mtahiniwa huyu aliandika majibu haya kwa sababu utunzi wa maswali unazingatia jedwali la utahini.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 2 (0.8%) tu ndio waliopata alama 6 hadi 10. Watahiniwa hao, walionesha uelewa wa wastani kuhusu aina za maswali. Hivyo, waliandika misingi sahihi miwili hadi mitatu kati ya mitano na kuandika kwa usahihi sehemu ya utangulizi na hitimisho linaloendana na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja mbili sahihi ambazo ni *kutunga swali la wazi lenye majibu ya moja kwa moja na kutokuchukua sentensi moja kwa moja kutoka kwenye kitabu* na kuchanganya na majibu mengine yasiyo sahihi. Hivyo, alipata alama 6.

### 2.2.4 Swali la 14: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali lilimtaka mtahiniwa afafanue namna ya kutumia kadi za maneno kufundishia aina za maneno katika hatua ya maarifa mapya na kukazia maarifa kwa kuonesha vitendo vya ujifunzaji na ufundishaji kwa kila hatua. Watahiniwa 258 (100%) walijibu swali hili. Kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ni cha wastani kwa kuwa asilimia 40.9 ya watahiniwa ndio waliopata alama 6 hadi 15. Chati Na. 12 inaonesha viwango vya ufaulu wa watahiniwa katika swali hili:




**Chati Na. 12:** Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 12


Chati Na. 12 inaonesha kuwa watahiniwa 153 (59.3%) walipata alama kuanzia 0 hadi 5.5, watahiniwa 95 (36.8%) walipata alama kuanzia 6 hadi 10 na watahiniwa 10 (3.9%) walipata alama kuanzia 10.5 hadi 15.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa asilimia 59.3 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama hafifu. Watahiniwa hao, walishindwa kuonesha namna ya kutumia kadi za maneno kufundishia aina za maneno kwa kuonesha shughuli za ufundishaji na ujifunzaji katika hatua ya maarifa mapya na kukazia maarifa. Wengi wao, walibainisha hatua zote za ufundishaji na kuelezea mwalimu anachopaswa kufanya katika kila hatua wakati wa kufundisha badala ya kujikita kwenye hatua ya maarifa mapya na kukazia maarifa. Hii inadhirisha kuwa, watahiniwa hawa wanazielewa vizuri hatua za ufundishaji lakini walishindwa kuonesha shughuli za ufundishaji na ujifunzaji kwa kuhusianisha na matumizi ya zana ya kadi za maneno wakati wa kufundisha aina za maneno.

Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo aliandika: *(i) Utangulizi:mwalimu kupima wanafunzi uelewa wao katika hiyo mada; (ii) Maarifa mapya:hapa mwalimu kukazia au kutoa maarifa mapya kwa kuwafundisha au kutoa maarifa ambayo wanafunzi hawana; (iii) Kukazia maarifa: Hapa mwalimu ataangalia achukue mbinu gani au zana gani ya kuwakilisha wanafunzi wajenge ubunifu; (iv) Tafakuri:Mwalimu atoe nukuu za somo ya mada hiyo ya aina za maneno na kuwapa maswali;* na *(v)Hitimisho:Mwalimu anatumia njia yoyote kuwapa nafasi wanafunzi kujieleza kitu gani walichokielewa*. Badala yake mtahiniwa huyo alipaswa kuandika *(i) maarifa mapya: shughuli ya ufundishaji ni: Kuongoza, kuchagua aina ya neno katika kadi zilizochanganywa* na *kitendo cha ujifunzaji: Kuchagua aina ya neno mfano nomino na kutaja aina za nomino* na *(ii) Kukazia maarifa mapya: shuguli ya ufundishaji ni kuongoza kutumia kadi kutofautisha aina nyingine za maneno na nomino* na *shughuli ya ujifunzaji ni kutofautisha kadi za aina za maneno mengine kama vivumishi, vitenzi viwakilishi na aina za nomino.*

Aidha, watahiniwa wengine walijibu kinyume na matakwa ya swali. Kati yao, walibainisha mbinu mbalimbali za kufundishia kama ifuatavyo: *Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo, ili kujua ni kwa kiasi gani mwanafunzi anauelewa na mada mpya; mbinu ya maswali na majibu ili kupima uelewa wa somo hilo, na mwisho kuwagawa wanafunzi katika*

*makundi ili waweze kufanya majadiliano* na wengine walifafanua aina mbalimbali za maneno kama vile: *vivumishi, viwakilishi, vielezi, nomino*, na *vitenzi*. Watahiniwa hawa, walitoa majibu haya kwa sababu mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji huhusisha matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji. Kwahiyo, kwa sababu swali linahusu ufundishaji na ujifunzaji, ilisababisha mtahiniwa kuelezea mbinu mbalimbali za ufundishaji. Aidha, walijibu aina mbalimbali za maneno kwa sababu walizingatia matumizi ya maneno *aina za maneno* katika swali hivyo, kupata alama 0. Kielelezo Na 14.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swahi hili kwa usahihi.


14 Vitendo vya ufundishaji - Ni hatua ya maendeleo ya somo ambayo huendaliwa na mwalimu lakini Vitendo vya ujifunzaji Ni hatua ya-maendeleo ya somo ambayo - mhusika ni Mwanafunzi.

Katika hatua za maanza mapya vitendo vya ufundishaji Mwalimu awape wanafunzi wajadili zana ya maneno. lakini vitendo vya ujifunzaji wanafunzi wajadili na watoe zana za maneno

Zifuatazo ni namna ya kutanya kwa kuonesha vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji.

Kuwagawa wanafunzi katika makundi kulingana na idadi yao Katika vitendo vya ufundishaji mwanafunzi anatakiwa kugawa wanafunzi katika makundi lakini katika vitendo vya ujifunzaji wanafunzi wanatakiwa wakae katika makundi.

Kuchagua kiongozi katika kila kikundi ili waongozwe katika mijadala. Katika vitendo vya ufundishaji lakini katika vitendo vya ujifunzaji wanafunzi washiriki kumchagua kiongozi na kumsikiliza.

Kuwapa maswali mbalimbali kuhusu aina ya maneno hayo. katika vitendo vya ufundishaji lakini katika-vitendo vya ujifunzaji wanafunzi washiri


**Kielelezo 14.1:** Sampuli ya sehemu ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 14.

Katika kielelezo Na. 14.1, mtahiniwa alifafanua hatua za kufuata iwapo mwalimu atafundisha kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi. Mtahiniwa alipaswa kuonesha vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji

katika hatua ya maarifa mapya na kukazia maarifa iwapo mwalimu atafundisha mada ya aina za maneno kwa kutumia kadi za maneno.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, asilimia 36.8 ya watahiniwa waliojibu swali hili walipata alama za wastani. Watahiniwa hao, walikuwa na uelewa wa wastani kuhusiana na namna ya kutumia zana za ufundishaji na ujifunzaji katika hatua mbalimbali za somo. Miongoni mwao, walielezea vitendo vingi vya ufundishaji na ujifunzaji lakini walishindwa kubainisha ni vitendo gani vipo katika hatua ya maarifa mapya na kukazia maarifa. Mathalani mtahiniwa mmoja aliandika hatua za kufundisha kama ifuatavyo: *(i) Kuwagawa wanafunzi katika makundi, kuwapa kadi zenye aina za maneno ili wabainishe aina za maneno katika kadi; (ii) Mwalimu atatoa kadi mojamoja ili kuwaonesha ili watambue aina za maneno katika kadi; (iii) Kuziandika aina za maneno walizozitaja;* na *(iv) Kutoa mazoezi kuhusu aina za maneno*. Aidha, watahiniwa wengine waliweza kujibu kwa usahihi katika hatua moja na kushindwa katika hatua nyingine. Hivyo, walipata alama za wastani.

Hata hivyo, watahiniwa wachache (3.9%) walipata alama 10.5 hadi 15 kwa sababu walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusiana na namna ya kutumia zana za ufundishaji na ujifunzaji katika hatua mbalimbali za somo. Hivyo, waliweza kuonesha vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji katika hatua ya maarifa mapya na kukazia maarifa iwapo mwalimu atatumia kadi za maneno kufundisha aina za maneno. Majibu sahihi yaliyoandikwa na watahiniwa wa kundi hili ni pamoja na: *(i) Maarifa mapya*. *Shughuli ya ufundishaji ni Kuongoza* na *kuchagua aina ya neno katika kadi zilizochanganywa* na *kitendo cha ujifunzaji ni kuchagua aina ya neno kama vile nomino na kutaja aina za nomino*. *(ii) Kukazia maarifa mapya: Shughuli ya ufundishaji ni kuongoza kutumia kadi kutofautisha aina nyingine za maneno na nomino* na *shughuli ya ujifunzaji ni kutofautisha kadi za aina za maneno mengine kama vivumishi, vitenzi viwakilishi na aina za nomino*. Kielelezo Na. 14.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu swali hili kwa usahihi.


14 Hatua ya maarifa mapya, hii ni hatua ya pili iliyopo katika jedwali la andalio la somo baada ya hatua ya utangulizi, ni hatua ambayo humtaka mwalimu kuonyesha ujuzi wake katika kufundisho somo, Kukazia maarifa, hii ni hatua ya tatu iliyopo katika jedwali la andalio la somo baada ya Maarifa mapya, yafuatayo ni maelekezo juu ya alichotakiwa kufanya mwalimu wa somo la Kiswahili katika kutumia kadi za Maneno katika ufundishaji (Maarifa mpya).

Kuwapatia wanafunzi kadi za maneno katika vikundi au kwa kila mmoja kama zipo za kutosha, wanafunzi watapatwa kuchunguza kadi hizo ili kubaini aina za maneno zilizoandikwa katika kadi hizo mmoja mmoja, jozi na kisha kama kundi zima.

Kuwapatia muda wanafunzi wa kuzichunguza kadi hizo ili kubaini aina za maneno, wanafunzi wanapaswa kuzichunguza kwa makini mmoja mmoja, jozi na kisha kundi zima na kuziandika aina za maneno walizoweza kuzipata baada ya kuchunguza kadi hizo.

Kuwapa wanafunzi nafasi ya kusema juu ya kile walichokichunguza kutoka kwenye kadi hizo, mfano wanafunzi watatakiwa kutaja aina za maneno walizochunguza kama vile nomino kitenzi na kivumishi kwa kila kundi na kisha mwalimu kutolea ufafanuzi zaidi juu ya aina za maneno walizochunguza na kutaja.

**Kielelezo 14.2:** Sampuli ya sehemu ya majibu sahihi katika swali la 14.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WATAHINIWA KWA MADA

Mtihani wa Stashahada ya Ualimu wa Sekondari wa Somo la Kiswahili ulikuwa na maswali kumi na nne (14) yaliyotungwa kutoka katika mada 11. Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa, watahiniwa wengi walijibu vizuri maswali yaliyotoka katika mada 7 ambazo ni *Vifaa vya Mtaala wa somo la Kiswahili (99.2%)*, *Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili (92.3%)*, *Maendeleo ya Kiswahili (83%)*, *Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili (80.1%)*, *Uhakiki wa Kazi za Fasihi (77.5%)*, *Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Kiswahili (73.3%)*, na *Fasihi (70.9%)*. Watahiniwa walifaulu vizuri katika mada hizi kwa sababu walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada hizo na kuelewa matakwa ya kila swali. Aidha, waliweza kujieleza kwa ufasaha na kufuata taratibu na kanuni za uandishi hasa katika maswali ya insha.

Kwa upande mwingine, ufaulu wa watahiniwa ulikuwa wa kiwango cha wastani katika mada 1 ya Zana za Kufundishia na Kujifunzia (69.4%) kutokana na baadhi ya watahiniwa kuandika majibu yasiyojitosheleza. Aidha, watahiniwa walipata ufaulu hafifu katika mada 3 ambazo ni Upimaji (39.4%), Ufahamu (32.2%) na Uandishi (10.5%).

Uchambuzi zaidi wa takwimu unaonesha kuwa mada ya *Vifaa vya Mtaala wa somo la Kiswahili*, *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*, *Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili*, *Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Kiswahili*, na *Fasihi* zimeendelea kuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa miaka miwili mfululizo (2022-2023), ingawa asilimia za ufaulu katika mada hizo zimeshuka kwa mwaka 2023. Mwaka 2022 mada hizo zilikuwa na ufaulu wa asilimia 99.3, 90.2, 88.9, 95.1 na, 94.1 na mwaka 2023 asilimia 99.2, 77.5, 83.5, 70. 9, 73.3 mtawalia. Vilevile, mada ya *Maendeleo ya Kiswahili* ndio mada pekee yenye kiwango kizuri cha ufaulu ambapo asilimia zimeongezeka kutoka 77.3 mwaka 2022 hadi asilimia 82.9 mwaka 2023.

Aidha, kiwango cha ufaulu kimeongezeka kwa asilimia 25.5 katika mada ya *Mbinu za Kufundisha somo la Kiswahili*. Mwaka 2022 mada hiyo ilikuwa na ufaulu wa asilimia 66.8 ilihali mwaka 2023 ni asilimia 92.3.

Vilevile, viwango vya ufaulu katika mada ya *Uandishi*, *Ufahamu* na *Upimaji* vimeshuka kwa asilimia 79, 55.6 na 19.5 mtawalia. Kwa mwaka 2022 mada hizo zilikuwa na ufaulu wa asilimia 89.5, 87.8 na 58.9 na mwaka 2023 asilimia 10.5, 32.2 na 39.4 mtawalia. Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu wa watahiniwa kimeshuka kwa asilimia 0.2 kutoka asilimia 99.8 mwaka 2022 hadi asilimia 99.6 mwaka 2023.

## 4.0 HITIMISHO

Kwa ujumla, taarifa hii inaonesha kuwa watahiniwa wengi wamefaulu somo la 721 Kiswahili kwa kiwango kizuri mwaka 2023 kwani asilimia 99.6 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani, walifaulu. Hii inadhihirishwa na ufaulu mzuri wa watahiniwa katika maswali 9 kati ya 14 katika mtihani mzima. Katika swali la 1, 2, 3, 4, 5, 6, 8, 10, 11, na 12, ufaulu ulikuwa wa asilimia 89.5, 92.9, 70.9, 99.2, 83.0, 73.3, 98.1, 77.6, 77.9, na 77.5 mtawalia. Utendaji huo, umetokana na watahiniwa kuelewa kwa kina mada zilizotahiniwa katika maswali hayo pamoja na matakwa ya swali.

Kwa upande mwingine, ufaulu haukuwa mzuri katika swali la 7, 9, na 13 ambapo ufaulu wa watahiniwa katika maswali hayo ulikuwa asilimia 32.2,10.5, na 0.8 mtawalia. Aidha, swali la 14 lilikuwa na utendaji wa wastani wa asilimia 40.7. Hivyo, juhudi zinahitajika katika kuimarisha uelewa wa mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia*, *Upimaji, Ufahamu*, na *Uandishi* ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu wa watahiniwa katika maswali yatakayotungwa kutoka katika mada hizo katika mitihani ijayo.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha zaidi kiwango cha ufaulu katika somo hili inashauriwa:

(a) Wizara inayohusika ione haja ya kuandaa warsha kwa wakufunzi ili waongezewe ujuzi katika mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia*, *Upimaji*, *Uandishi* na *Ufahamu*. Hii itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu katika maswali yanayotungwa kutoka katika mada hizo na kuwafanya watahiniwa kuleta tija kwa taifa mara tu watakapoanza kazi.

(b) Wakufunzi watumie matini ya mfano wa hotuba na iliyorekodiwa katika kufundisha uandishi wa hotuba kwa kuzingatia aina zake ili kuinua ufaulu katika mada ya *Uandishi*.

(c) Katika kufundisha mada ya *Ufahamu*, wakufunzi watumie zana za matini, magazeti, na vijarida ili wanachuo waweze kubaini kwa urahisi umuhimu wa kufundisha somo hilo kwa wanafunzi wao.

(d) Wakufunzi watumie mbinu ya bungua bongo, onesho mbinu, majadiliano ya vikundi na mazoezi katika kufundisha mada ndogo ya *Kutunga Maswali ya Mtihani*.

(e) Wakufunzi wawaandalie wanachuo mazoezi ya kutosha ya kuandaa aina mbalimbali za maswali kwa kuzingatia misingi yake ili waweze kuielewa na kuitumia kwa urahisi wakati wa utunzi wa maswali hayo. Hii itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu katika mada ndogo ya *Kutunga Maswali*.

(f) Wakufunzi watilie maanani katika kuwafundisha na kuwasisitiza wanachuo juu ya matumizi sahihi ya alama za uakifishaji sambamba na uandishi wa insha zenye mtitririko wenye kuleta mantiki. Hii itazidi kuchochea kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa ambao wamepata alama pungufu kwa kuandika insha zisizo na mtiririko mzuri.

**KIAMBATISHO CHA PEKEE**

## UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA

| Na | Mada | Namba ya swali | Viwango vya Kufaulu (%) | | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | 40 na Zaidi | Wastani | |
| 1. | Vifaa vya Mtaala wa Somo la Kiswahili | 4 | 99.2 | 99.2 | Vizuri |
| 2. | Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Kiswahili | 2 | 92.3 | 92.3 | Vizuri |
| 3. | Utumizi wa Msamiati na Miundo ya Kiswahili | 1 | 89.5 | 83.5 | Vizuri |
| | | 12 | 77.5 | | |
| 4. | Maendeleo ya Kiswahili | 5 | 83.0 | 83.0 | Vizuri |
| 5. | Uhakiki wa Kazi za Fasihi | 11 | 77.6 | 77.6 | Vizuri |
| 6. | Maandalizi ya Ufundishaji wa Somo la Kiswahili | 8 | 73.3 | 73.3 | Vizuri |
| 7. | Fasihi | 3 | 70.9 | 70.9 | Vizuri |
| 8. | Zana za Kufundishia na Kujifunzia | 6 | 98.1 | 69.4 | Wastani |
| | | 14 | 40.7 | | |
| 9. | Upimaji | 10 | 77.9 | 39.4 | Hafifu |
| | | 13 | 0.8 | | |
| 10. | Ufahamu | 7 | 32.2 | 32.2 | Hafifu |
| 11. | Uandishi | 9 | 10.5 | 10.5 | Hafifu |